# UYAKINIFU WA MAUDHUI MAKUU KATIKA UTENZI WA ABDIRRAHMANI NA SUFIYANI

NA

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

KIPTUM JERUTO TECLA
NAMBARI YA USAJILI: C50/72353/2014

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

A1701243A
University of Nairobi Library Thesis
2016

MWAKA: 2017

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile.

Sahihi.......................................... Tarehe 16TH NOV. 2017.

Kiptum Jeruto Tecla

C50/72353/2014

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi.......................................... Tarehe 16/11/17

Prof. Kineene wa Mutiso

(Msimamizi)

Prof. Rayya Timammy

(Msimamizi)

Sahihi.......................................... Tarehe 16th NOV 2017

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu wapendwa Bw. na Bi. Pius Kiptum nawashukuru kwa kunilea na kujukumika katika safari yangu ya kusaka elimu bila kukata tamaa. Nawapa shukrani kaka na dada zangu walionitia motisha ya kuweza kuafikia maazimio yangu kimasomo. Namshukuru mume wangu Bw. Silas Koome kwa kunifaa kwa hali na mali nilipopungukiwa na jambo tangu nilipoanza masomo yangu katika ngazi ya uzamili hadi tamati. Kwa watoto wangu wapendwa Clara Kendi na Austin Muriki, nawashukuru sana kwa kuvumilia upweke uliotokana na safari zangu za kila mara chuoni. Mungu awabariki.

# SHUKURANI

Ningependa kumshukuru Rabana kwa kunipa siha nzuri ya kuweza kuhitimu ngazi hii ya elimu. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Kineene wa Mutiso na Prof. Rayya Timammy kwa uelekezi wao mzuri walionipa katika hatua zote za uandishi wa tasnifu hii. Jalali awabariki, awaongezee hekima , busara na ujuzi zaidi katika kazi zao.

Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa kunipa maarifa yaliyochangia sana kuafikia malengo yangu kielimu. Wahadhiri hao ni kama vile : Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Jefwa Mweri na wengine.

Namshukuru mwanafunzi mwenzangu Florence Mutheo kwa kunifaa katika harakati zangu za kusaka elimu katika ngazi ya uzamili. Vilevile nawapa kongole wanafunzi wenzangu tuliong'ang'ana pamoja usiku na mchana kuhakikisha kuwa malengo yetu yameafikiwa hasa katika ngazi hii ya uzamili. Mola awabariki popote mlipo.

# IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia uchambuzi wa maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwa kusoma utenzi wenyewe na kudondoa yale masuala mazito yenye uyakinifu katika maisha ya jamii. Tumeongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii katika kuchanganua maudhui haya makuu yaliyojitokeza wazi katika jamii ya jadi na pia katika jamii ya sasa. Maudhui haya ni kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano. Tuliweza kuoanisha masuala haya na nadharia ya uyakinifu wa kijamii kwani kulingana na mihimili yake, masuala yanayoelezwa katika utenzi wetu, yanazingatia hali halisi yanayoikumba jamii katika vigezo vitatu: kisosholojia, kiuchumi na kisiasa. Vilevile jamii hutathmini maendeleo yake kutokana na vigezo hivi ili iweze kupiga hatua. Tuliweza kusoma kazi mbalimbali zinazohusiana na utenzi ili kupata mwelekeo mzuri wa kutusaidia kufanya uchambuzi wa maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kama kazi yetu husika. Tumewasilisha masuala tuliyoyachanganua kupitia maelezo na ufafanuzi mwafaka kwa kuonyesha jinsi maudhui haya yanavyoweza kuleta matokeo hasi na chanya katika jamii ya sasa. Kutokana na utathmini wetu, tumedhihirisha wazi kwamba dini ndilo suala kuu linalozaa masuala au maudhui mengine tuliyoyachambua kama vile usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano. Mtagusano wa wanajamii huleta tofauti mbalimbali katika jamii kwa mfano tofauti za kidini huleta vita, usaliti na dhuluma miongoni mwao. Vilevile utangamano mzuri hufanya jamii kuishi katika ndoa iliyo na mapenzi na ambayo hujenga uhusiano mwema katika jamii kupitia dini.

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **K.L.B.** | Kenya Literature Bureau |
| **n.k.** | na kadhalika |
| **n.w.** | na wenzake |
| **S.O.A.S.** | School of Oriental and Africa Studies |
| **ub.** | ubeti |

# YALIYOMO


**UNGAMO** ........ ii

**TABARUKU** ........ iii

**SHUKURANI** ........ iv

**IKISIRI** ........ v

**VIFUPISHO** ........ vi

**YALIYOMO** ........ vii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

1.0 Utangulizi ........ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........ 3

1.3 Nadharia Tete ........ 3

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........ 4

1.5 Upeo na Mipaka ........ 4

1.6 Misingi ya Kinadharia ........ 5

1.6.1 Mihimili ya Nadharia ........ 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Fasihi ........ 7

1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Tenzi ........ 8

1.8 Mbinu za Utafiti ........ 13

1.8.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli ........ 13

1.8.2 Ukusanyaji Data na Mbinu za Ukusanyaji Data ........ 13

1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ........ 14

1.9 Hitimisho ........ 14

**SURA YA PILI** ........ 15

**VIAMBAJENGO VYA MAUDHUI** ........ 15

2.0 Utangulizi ........ 15

2.1 Dhana ya Mtindo ........ 15

2.1.1 Wahusika ........ 15

2.1.2 Mandhari ........ 18

2.1.3 Msuko ........ 20

2.1.4 Sauti ya Usimulizi ........ 21

2.2 Hitimisho ........ 23

**SURA YA TATU** ........................................ **24**
**MAUDHUI MAKUU KATIKA UTENZI WA ABDIRRAHMANI NA SUFIYANI** ........................................ **24**
3.0 Utangulizi ........................................ 24
3.1 Dini ........................................ 24
3.1.0 Uislamu na Ukafiri ........................................ 25
3.1.1 Uislamu ........................................ 25
3.1.2 Ukafiri ........................................ 31
3.1.3 Usaliti na Dhuluma ........................................ 32
3.1.4 Ndoa na Mapenzi ........................................ 37
3.1.5 Ushujaa / Ubabe ........................................ 39
3.1.6 Vita ........................................ 46
3.1.7 Maridhiano ........................................ 54
3.2 Hitimisho ........................................ 56
**SURA YA NNE** ........................................ **58**
**KUTATHMINI UYAKINIFU WA MAUDHUI MAKUU KATIKA UTENZI WA ABDIRRAHMANI NA SUFIYANI KATIKA JAMII YA SASA** ........................................ **58**
4.0 Utangulizi ........................................ 58
4.1 Dini ........................................ 58
4.1.1 Usaliti na Dhuluma ........................................ 64
4.1.2 Ndoa na Mapenzi ........................................ 66
4.1.3 Ushujaa ........................................ 67
4.1.4 Vita ........................................ 70
4.1.5 Maridhiano ........................................ 70
4.2 Hitimisho ........................................ 71
**SURA YA TANO** ........................................ **72**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........................................ **72**
5.0 Utangulizi ........................................ 72
5.1 Muhtasari wa Utafiti ........................................ 72
5.2 Matokeo ........................................ 72
5.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ........................................ 73
**MAREJELEO** ........................................ **74**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kupitisha ujumbe uliokusudia kwa hadhira. Fasihi ni sanaa sawia na sanaa zingine kama vile ufinyanzi, uchongaji, uchoraji na uimbaji ambazo huhitaji ujuzi wa binadamu ili kufanikisha kazi hiyo. Sanaa hii ya fasihi ina tanzu mbili yaani fasihi andishi na fasihi simulizi. Asili au chanzo cha fasihi andishi ni fasihi simulizi kwani simulizi ilianza mwanzo kabla ya uandishi. Tanzu za fasihi andishi ni kama vile tamthiliya, riwaya, mashairi, wasifu, tawasifu na nyinginezo. Vilevile fasihi simulizi ina tanzu zake kama vile ngano, hadithi, maigizo n.k.

Katika utafiti wetu, tumejikita kwenye ushairi ambao ni utanzu wa fasihi andishi. Ushairi huwa na dhima mbalimbali katika jamii kama vile kuhifadhi mila na desturi za jamii, kuonya, kuelimisha, kuadilisha, kuburudisha n.k. Imekuwa dhahiri shahiri kwamba, kazi nyingi za fasihi zimetungwa ili kulenga kuadilisha jamii kwa jumla sawia na *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ambao umejikita katika kuadilisha jamii dhidi ya maovu kupitia dini ya Kiislamu. Dini ni chombo cha kubadilisha hulka hasi kuwa njema ili kuleta muamana mzuri miongoni mwa wanajamii. Uhusiano huu ndio hujenga utu kwa binadamu.

*Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ulitungwa na Hemedi Bin Abdalla katika kipindi cha utasa katika historia ya ushairi. Utenzi huu una beti 1000 na ulitungwa kati ya miaka ya 1885-1945 wakati ambapo maandishi ya fasihi ya Kiswahili kwa ujumla yalikuwa machache. Kipindi hiki ndicho kulikuwa na ujio wa wageni kutoka mataifa ya Ulaya waliokuja kung'ang'ania bara la Afrika.

Utafiti wetu unahusu maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Utenzi ni aina ya ushairi wa kimapokeo wenye maudhui yanayosimulia kwa urefu tukio fulani maalum kama vile wasifu wa mtu au jambo la kihistoria kwa mfano *Utenzi wa Vita vya Uhuru* unaohusu historia ya nchi na *Utenzi wa Mapenzi Bora* unaohusu sifa za mapenzi bora.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa utendi ni ushairi wa kishujaa ambao huchukua sura ya masimulizi na kuwa na mgogoro mkali pamoja na mtindo sahili katika kisa ingawa wahusika wanaohusika katika matukio hayo huweza kuwa wengi mno.

Utafiti huu unalenga kuangazia maudhui makuu yanayohusiana na maisha ya binadamu ulimwenguni katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Mbatiah (2010) anasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Tunakubaliana na haya mawazo ya Mbatiah kwa kusema kuwa maudhui ni mambo makuu yanayojitokeza katika kazi yoyote ile ya fasihi ambayo mwandishi anaikuza kulingana na uwezo wake. Wamitila (2008) anasema kwamba maudhui huweza kuelezwa kwa njia mbili zinazohusiana kimsingi kwa sababu ni dhana pana. Njia ya kwanza ni kuwa maudhui huweza kuelezwa kama jumla ya masuala yote yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi kutegemea na jinsi mwandishi anavyoikuza mada yake; pili, maudhui yametumiwa kurejelea kiwango cha maana cha matini au kazi ya fasihi husika.

Mwandishi wa *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* Hemedi Bin Abdalla amesawiri masuala mbalimbali yanayomzingira na kumwongoza binadamu. Ameangazia suala kuu ambalo ni dini ya Kiislamu hasa kwa kuonyesha nguvu zinazompa Mungu uwezo mkubwa dhidi ya nguvu hafifu za miungu. Historia hii inahusu dini ya Kiislamu kwa kumulika mhusika Abdirrahmani mwanawe Abubakari aliyepotea akiwa na umri mdogo kwenda kuishi nchi nyingine na kiongozi aliyeitwa Sufiyani. Abdirrahmani aliaminika sana kiasi cha kupewa mamlaka na hata kuozwa bintiye Sufiyani. Himaya ya Sufiyani iliishi kwa kuamini miungu tofauti na himaya aliyokulia Abdirrahmani. Abdirrahmani na Sufiyani walitawala katika uongozi uliojaa maovu mengi hadi wakati ambapo Abdirrahmani aliamua kuasi utawala wa Sufiyani na kutoroka kwenda kwao Madina kutokana na msukumo wa babake ambaye hakufurahishwa na matendo yake; Vita vya kidini vilizuka baina ya waamini Mungu (Abdirrahmani) na miungu (Sufiyani) ndiposa nguvu za Mungu zikadhihirisha uwezo mkubwa wa kutenda miujiza zaidi dhidi ya nguvu za miungu.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Maudhui kama jumla ya masuala yote yanayozingira maisha ya kila binadamu duniani, hivyo inakuwa ni lazima jamii ifahamu mambo kama vile dini, uongozi mbaya, vita na mengineyo ambayo yalifanyika, yanaendelea kufanyika na yatafanyika siku zijazo katika jamii yoyote ile bila kubagua watu na nchi zao. Vita vya kidini vinaendelea kushuhudiwa katika jamii ya sasa kwa sababu ya uongozi mbaya katika taasisi zetu. Kutokea kwa masuala haya ni thibitisho wazi kuwa jamii ina upungufu wa elimu kuhusu masuala yanayogusia maisha yao ya kila siku kiuchumi, kisiasa na kisosholojia ndio maana watu wanaathirika kila uchao bila kupata funzo kutokana na mienendo yao hasi.

Tatizo la utafiti wetu ni kuchambua maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kama vile: dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano ili kupitia usomaji wake, jamii ya sasa iweze kupata mafunzo ya kuleta mabadiliko dhidi ya masuala yanayoathiri jamii. Jamii inaweza kuiga athari chanya na kuepuka athari hasi zinazoweza kuleta uhasama miongoni mwao.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

1. Kuchanganua maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.*
2. Kutathmini uyakinifu wa maudhui haya katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* katika jamii ya sasa.

## 1.3 Nadharia Tete

1. Mtunzi wa *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* amesawiri maudhui ya dini kama suala kuu linalozaa maudhui mengine kama vile: usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano.
2. Maudhui ya dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano ni elementi zenye uyakinifu zinazojitokeza katika jamii ya sasa.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Tumechagua mada hii kwa sababu zifuatazo:

Kulingana na utafiti wetu wa maktabani, hatujakumbana na kazi zozote zile zilizochambua maudhui katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* isipokuwa katika tenzi zingine kama vile *Utenzi wa Mwanakupona*, *Utenzi wa Mwana Fatuma* na *Utenzi wa Nabii Issa.* Wataalamu na wahakiki wengi wameshughulikia tenzi mbalimbali kwa kuchanganua dhana ya maudhui na fani lakini *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* haujachambuliwa isipokuwa katika utafsiri wake kutoka lugha ya Kiarabu hadi lugha ya Kiswahili na pia lugha ya Kiingereza ndio maana tumepata pengo la kufanyia utafiti wetu.

Tumechagua kuchambua maudhui makuu kwa sababu yanaonekana katika maisha halisi ya binadamu duniani. Dini kama mfano ni suala muhimu mno linalotawala maisha ya kila binadamu katika matendo yao ya kila siku, imeangaziwa kwa mapana na marefu ndio maana pasi dini binadamu si chochote duniani.

Tumeamua kuchagua mada hii ya maudhui makuu kwa minajili ya kuweka msingi kwa watafiti wengine watakaotafitia mada zinginezo katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Uhakiki huu wa *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* utawapa mwongozo na pengo la kuangalia mada zinginezo kama vile fani.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti wetu umejikita katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* na ambao tumeangazia maudhui makuu hasa kwa kuchambua masuala kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano miongoni mwa wahusika na wala sio mtindo katika utenzi.

Tumejikita katika nadharia ya uyakinifu wa kijamii ambayo inalenga kusawiri jamii katika hali ya uyakinifu. Mihimili ya nadharia hii imesisitiza kuhusu mabadiliko ambayo jamii inafaa kupigania ili kuleta usawa wa kiuchumi, kisiasa na kisosholojia katika jamii iliyogawika kwa msingi wa kitabaka. Aidha, hatua za kimaendeleo ambazo jamii imepiga kihistoria huangaziwa katika nadharia hii.

## 1.6 Misingi ya Kinadharia

Tumetumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii kama mwongozo wetu wa kuchanganua maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Nadharia hii iliasisiwa na Stalin mwaka wa 1917. Stalin aliishi miaka ya 1878-1953. Msukumo wake wa kutaka kubadilisha jamii ya Urusi ulichangiwa mno na mawazo ya Maksi hasa alipokuwa mhazili wa Chama cha Ujamaa (Russian Communist Party). Alihamasisha jamii pamoja na mwanamapinduzi mwenzake Lenin; Malengo yao makuu yakiwa kuzindua tabaka la chini la wanaonyanyaswa ili kufahamu na kutetea haki zao dhidi ya tabaka la juu la mabepari. Stalin alitumia mwongozo wa nadharia ya umaksi ili kuonyesha uyakinifu wa maisha kwa kuleta usawa Urusi kupitia mapinduzi dhidi ya wachache waliotawala masuala ya kiuchumi, kisiasa na kisosholojia.

Istilahi hii ya uyakinifu wa kijamii ilipata mchango mkubwa kutoka kwa wahakiki wengine baada ya uasisi wake na miongoni mwao ni pamoja na Lucaks (1963) na Gorky (1973). Lucaks (1963) anaeleza kuwa uyakinifu wa kijamii ni nadharia inayosawiri hali halisi ya jamii na hatua ambazo jamii imechukua katika mabadiliko yake hasa kisosholojia. Jamii hupata msukumo fulani ambao huleta mabadiliko hasa wahusika wanapokumbwa na ubaguzi fulani kama vile wa kisiasa, kiuchumi na kisosholojia. Vilevile, Lucaks (1963) alichangia katika kuimarisha mawazo ya Maksi alipokuwa akihudumu katika baraza la magazeti la *'Literacy Critic'.* Nadharia hii imetufaa katika kuchanganua maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwani jumla ya masuala yanayogusiwa yanaleta uyakinifu wa maisha.

Gorky (1973) anaeleza uyakinifu wa kijamii kama mwonoulimwengu wa watu wanaoubadilisha na kujenga upya ulimwengu. Jamii ina jukumu la kuleta maisha mapya katika vipengele vyote vinavyohusu binadamu kama vile uchumi, siasa n.k.Vilevile Brecht (1973) ameeleza kuhusu nadharia hii ya uyakinifu kwa kusema kuwa ni sanaa ya mapambano ambayo inapambana na mawazo ya uongo kuhusu hali halisi ya jamii pamoja na hisia za kuleta hujuma katika maslahi ya binadamu. Kulingana na nadharia hii, utabaka unaangaziwa hasa katika hali ya kunasua wanyonge kutoka kwa minyororo ya tabaka la juu ili waweze kujikomboa na kuleta mabadiliko katika jamii wanamoishi. Anatumia pia wahusika husika kuigiza nafasi ambazo zinawakilisha jamii halisi inayozalisha uchumi kama vile wakulima ili kuleta mabadiliko na kuondoa utabaka kupitia mapinduzi. Brecht (1973) anaamini kuwa

jamii itakapozinduka na kupata ukweli wa mambo halisi, itaweza kuleta usawa kwa wote 'class consciouness' hivyo basi alitumia maneno yake kuwa silaha ya ukombozi kwa jamii. Mawazo haya yote ya waasisi tuliowataja hapo juu yametufaa katika kuchanganua masuala yanayokumba maisha ya wanajamii.

Senkoro (1987) anachangia mawazo yake kuhusu nadharia ya uyakinifu wa kijamii kwa kusema kuwa ni kiwango cha juu cha uhakiki wa uhalisia. Anaeleza pia kuwa binadamu ndiye nguzo kuu ya kuleta utabaka katika jamii na kwa hivyo anasisitiza kuwa masuala yote yanayohusiana na binadamu yasifichwe bali yawekwe wazi ili mabadiliko yaweze kufanyika.

Wamitila (2003) anaeleza kuhusu uyakinifu wa kijamii kwa kusema kuwa ni nadharia inayosisitiza umuhimu wa uhalisia ambao hutilia mkazo hatua za kimaendeleo hasa za kihistoria. Hatua zote za kimaendeleo za binadamu huwa na umuhimu wake katika kueleza yanayotendeka katika jamii ya sasa. Vilevile Wafula na Njogu (2007) wanachangia mawazo yao kwa kueleza kuwa binadamu ana umuhimu mkubwa ulimwenguni kwani ndiye huchangia pakubwa katika kuwepo kwa ulimwengu na maana yake.

### 1.6.1 Mihimili ya Nadharia

Nadharia ya uyakinifu wa kijamii huongozwa na mihimili ifuatayo:

1. Nadharia hii husawiri jamii katika ukamilifu wake na kuonyesha hatua za jamii kimaendeleo.
2. Huzingatia hali halisi ya jamii na kuitumia kueleza namna jamii inavyoelekea kwenyeusoshiolisti.
3. Pamoja na kusawiri matukio ya kihistoria, wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka. Tabaka la wanyonge hujifungata masombo kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi.
4. Wahusika huonyeshwa kiuyakinifu.Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Fasihi

Kwa mujibu wa Achieng (2012) akielezea mawazo ya Abraham (1971) ni kuwa kazi za fasihi nyingi zinazosawiri sifa bia zenye vipengele vyote vya maisha ya binadamu wote vinavyosaidia katika kukomboa jamii dhidi ya hali dhalilishi. Maoni haya yanatufaa pakubwa katika kuchanganua maudhui yanayogusia hali halisi ya maisha ya binadamu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kama vile dini, usaliti na dhuluma miongoni mwa masuala tuliyayoshughulikia katika kazi yetu.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa fasihi huwa na sifa bia zinazozipa sifa za kiulinganishi. Anashikilia kuwa msingi wa fasihi ni jamii kwani jamii hujengwa na binadamu ndiposa jamii yote huwiana katika masuala yanayohusu maisha ya waja wote kwa jumla. Fasihi ni kioo cha jamii na ndio maana huchota malighafi yake kutoka kwa jamii, hii ina maana kuwa yale yanayozingira binadamu wote yanafanana ulimwenguni. Mikinzano inayopatikana katika jamii ndio husababisha migawanyiko ya jamii kisiasa, kiuchumi na kisosholojia. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umeonyesha uwiano wa mambo halisi yanayotendeka katika mazingira yetu kama yanavyoelezwa na Wamitila (2003). Masuala haya ya kiuyakinifu ni kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano miongoni mwa wahusika.

Achieng (2012) anaeleza maoni ya Mutiso (1999) kuwa binadamu wote ni sawa popote walipo ingawa kuna tofauti ndogo ndogo za kufikirika zinazosababishwa na tofauti za kimazingira na kihistoria kwa hiyo fasihi humulika masuala yanayoshabihiana ulimwenguni bila kubagua binadamu wenyewe. Maelezo haya yamekuwa ya manufaa kwetu kwani masuala yanayoangaziwa katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* yana uhusiano na masuala yanayomkumba binadamu yeyote pale tofauti ikiwa tu ni mazingira na wakati katika historia ambao hadithi yenyewe ilisimuliwa. Mambo haya yanayoelezwa yanahusu maisha ya binadamu halisi kama vile dini, ndoa na mapenzi, usaliti na dhuluma, ushujaa, vita na maridhiano.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Tenzi

Mada yetu kuhusu maudhui makuu imejikita katika ushairi wa Kiswahili wa jadi kama msingi wetu. Tumerejelea mashairi yaliyoandikwa kabla ya karne ya ishirini kwa sababu tenzi nyingi enzi hizo zilibeba maudhui ya dini ndiposa mada yetu ikapata kurunzi ya kurejelea suala hili la dini kama mojawapo wa maudhui tuliyoshughulikia. Tendi nyingi zimeangazia masuala ya dini hasa dini ya Kiislamu. Dini ya Kiislamu katika tenzi nyingi za Kiswahili imeangaziwa na sio kwa sababu asili yake ni barani Afrika bali ilienezwa tu barani Afrika kupitia waarabu katika shughuli za kibiashara hivyo basi dini hii sawia na dini ya Kikristo ni dini zilizoletwa na wageni kwa mfano asili ya dini ya Kiislamu ni barani Asia.

Watalaamu wa kigeni waliofanya utafiti katika tenzi za jadi au za kale ni kama wafuatao: Knappert (1967, 1971 & 1979) na Harries (1962). Licha ya uchunguzi wa kina katika tenzi hizi za kale, Kezilahabi (1997:59) aliwapuuza wataalamu hawa wa kigeni kwa kusema,

> "......wale wataalamu wa kizungu ambao wamejitahidi sana na kukiendeleleza na kukikuzaKiswahili walikuwa na ujuzi mdogo sana wa fasihi. Wao walikuwa wataalamu wa lugha na hawakuweza kufanya lolote zaidi ya kukusanya maandishi kadha ya Kiswahili na kutafsiri katika lugha zao kwa manufaa yao wenyewe kwa upande wa lugha, walifanya mambo mengi mazuri".

Wahakiki hawa wa kigeni hawakutambua tofauti ya dini ya Kiislamu hasa katika itikadi zao na utamaduni wa Kiswahili pamoja na waislamu wenyewe katika maeneo ya Afrika mashariki. Uchunguzi wao ndio ulipelekea mchango wake Trimingham (1962) ambaye alieleza kuwa mtu yeyote aliyesilimu aliendelea kuwa mwafrika hata kama alipaswa kufuata mbeko za Uislamu kama vile *"faradhi na sunna"* Thibitisho mwafaka la usemi huu lilidhihirika wazi katika kazi zao za usanii na uandishi zilizojumuisha utamaduni wa kiafrika kama vile nyimbo za jandoni, unyagoni, tenzi na mashairi kadha wa kadha. Maelezo haya yametusaidia katika kuelewa na kuchanganua maudhui ya dini ya Kiislamu kwa kuangazia sheria na nguzo za dini hii zinazomwongoza binadamu hasa katika matendo yake ulimwenguni kwa mfano 'swala'.

Abdalla (1891) ametunga *Utenzi wa Vita vya Wadachi* kutamalaki mrima ambao ulionyesha historia ya jamhuri ya Tanganyika kwa kutumia vigezo vya dini hasa dini ya Kiislamu. Suala la kuabudu Mungu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo linatiliwa mkazo hasa kwa kuwakinga waumini wake kutokana na majanga ya aina yote na maadui wabaya. Kuamua kujihusisha na utenzi huu wa kidini ni kwa sababu umetufaa sana hususan katika kuambatanisha na mada yetu ya maudhui ambayo ni suala la dini ingawaje unatofautiana pale ambapo *Utenzi wa Vita vya Wadachi* unaangazia kipindi cha ung'ang'aniaji wa uhuru katika nchi ya Tanganyika ilhali *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umejikita katika kipindi cha kuenea kwa dini ya Kiislamu kwani wahusika wengine wanaonyeshwa wakiwa katika harakati ya kusaka Uislamu.

Kijumwa (1926) katika *Utenzi wa Siraji* anaeleza kuhusu kujenga uhusiano mwema na majirani, watu wa ukoo na marafiki kupitia dini. Anamshauri mwanawe Helewa kuwa azingatie sana masuala ya dini na mawaidha ya jamii. Ushauri huu wa Kijumwa kwa kijana wake umetufaa pakubwa katika kuoanisha matukio katika utenzi wetu *naUtenzi wa Siraji.* Abdirrahmani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* anapata ushauri kutoka kwa babake Abubakari wa kumtaka kuacha kunyanyasa wapita njia ili kumwezesha kujenga uhusiano mwema na Mungu na jamii kwa jumla. Utenzi wetu umetofautiana na *Utenzi wa Siraji* pale ambapo maudhui ya ukafiri na vita yanajitokeza miongoni mwa wahusika wakuu na ambayo *Utenzi wa Siraji* haukusawiri masuala haya.

Robert (1966) katika *Utenzi wa Adili* anaeleza kuhusu umuhimu wa kuwa na maadili katika maisha ya binadamu. Anasema kuwa kumcha Mungu ndiyo jambo la muhimu linalomwelekeza binadamu kuwa na heshima kwa wazazi, kuwa na mapenzi ya dhati katika ndoa n.k. Maelezo haya yanayohusu dini yanaafikiana na kazi yetu ya utafiti kwani suala la dini limechambuliwa kama chombo cha kuadilisha jamii ili kuepukana na maovu kwa mfano mhusika Abdirrahmani anabadili imani yake ya kuamini miungu na kufuata imani ya Uislamu inayoamini Mungu mmoja pekee. Abdirrahmani anaacha unyanyasaji na kuwa mtu mwema kupitia dini. Vilevile wosia wake Shaaban kwa mwanawe wa kiume ni wa kumshauri awe na mapenzi ya dhati katika ndoa. Maelezo haya yanaleta uhusiano wa karibu na kazi yetu kwani suala la ndoa limejitokeza kwa wahusika wachache katika utenzi wetu kwa mfano kuna ndoa baina ya Abdirrahmani na binti Sufiyani na ndoa baina ya Abubakari na mkewe.

Mapenzi katika ndoa ya wahusika hawa yameimarishwa na dini ya Kiislamu hivyo basi kuamini Mungu huleta amani katika jamii kwani Mungu ni mwenye kutoa amani kulingana na sifa ya Mungu katika dini ya Kiislamu.

Robert (1968) amesawiri suala la dini katika utunzi wake wa riwaya ya *Utubora Mkulima* kwa kusisitiza maadili yanayojenga mtu. Robert (1968) amebainisha wazi kuwa dini hasa ya Kiislamu huleta mafanikio kwa anayeamini uwezo wa Mungu hivyo basi dini ya Kiislamu imetufaa katika kuchanganua maudhui ya dini katika kazi yetu kwani dini ndio chanzo cha maadili. Vilevile dini ndio suala linalozaa masuala mengine kama vile uaminifu, ndoa na mapenzi n.k.

Biebuyck na Mateene (1969) wanaaangazia mada ya dini hasa katika kueleza kuhusu jagina au shujaa Mwindo aliyeishi kwa kutumia nguvu za kichawi. Walimulika maisha yake na jinsi alivyokuwa akimwomba mungu wa radi (Nkuba) ampe uwezo wa kupambana na watu wa Tubondo. Sifa za Mwindo za kiajabu za kuwa na uwezo mkubwa wa kutenda mambo zilielezwa hasa akiwa tumboni mwa mamake. Suala la dini limeangaziwa kwa kuonyesha jinsi jamii hiyo ilivyotegemea nguvu za miungu pamoja na shujaa wao sawia na kazi tunayoifanya ambayo dini inahusishwa na nguvu za Mungu katika kutenda miujiza miongoni mwa wahusika kama vile Abdirrahmani na pia nguvu za miungu ziliangaziwa kwa mhusika Sufiyani lakini hazikuwa na uwezo wa kutenda miujiza yoyote katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* hivyo kutupa mwongozo mwafaka wa kutathimini nguvu za dini ya kweli na ya uongo.

Abdilatif (1973) ameangazia *Utenzi wa Fumo Liyongo* uliotungwa na Kijumwa kwa kueleza kuhusu shujaa aliyekuwa na sifa zisizo za kawaida hasa katika maumbile yake pamoja na nguvu za kufanya mambo ambayo binadamu wa kawaida hangeweza kufanya. Kutokana kimo chake kisicho cha kawaida aliweza kutembea safari iliyochukua binadamu wa kawaida siku nne, Liyongo akichukua siku mbili. Vilevile nguvu zake nyingi zilimwezesha kubeba vitu vingi kwa wakati moja. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* una sifa za majagina kama vile mtume Muhammadi alivyokuwa na nguvu zisizo za kawaida hata kutuma uponyaji wa papo kwa hapo kwa Abdirrahmani alipokuwa amejeruhiwa vitani. Utenzi huu wa kishujaa umetufaa katika kuelewa zaidi sifa za wahusika waliosawiri ubabe katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.*

Mayoka (1978) ameangalia suala la dini ya Kiislamu katika *Utenzi wa Vita vya Uhuru wa Msumbiji* ambapo dhana ya dini imewekwa mbele hasa katika harakati za kujinasua kutoka minyororo ya ukoloni. Ukombozi wao ulitegemea mapenzi ya Mungu kupitia maombi yao. Vilevile utenzi wetu umemweka Mungu mbele katika vita vya kiroho na vya kimwili ambavyo mhusika kama Abdirrahmani alivipitia akijikomboa kutoka kwa kiongozi katili Sufiyani. Tumetofautiana na *Utenzi wa Vita vya Uhuru wa Msumbiji* kwani maudhui yake yalisawiri kipindi cha ukombozi wa nchi ya Msumbiji ilhali maudhui katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* yamedhihirisha kipindi cha maenezi ya dini ya Kiislamu.

Mghanga (1984) katika tasnifu yake ya uzamili ameangazia hadithi tano za jamii ya Kidawida. Alifanya uchambuzi wa maudhui katika ngano hizo kwa kuonyesha uhusiano wa maudhui yao. Uchanganuzi huu wa maudhui una uhusiano wa karibu na kazi yetu kwani tumejihusisha na maudhui katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kama mada yetu katika utafiti. Mghanga (1984) amechanganua maudhui ya ubinafsi katika hadithi ya sungura na ndovu kwa kutumia wahusika husika hivyo kutufaa katika uchanganuzi wetu wa maudhui.

Wa Mutiso (1985) amemulika *Utenzi wa Hamziyyah* (mama wa miji) na ambao suala la dini linajitokeza kuhusu maisha ya mtume Mohammadi ambaye ni mtume wa mwisho kulingana na dini ya Kiislamu. Tumeamua kurejelea utenzi huu katika utafiti wetu kwani pia suala la mtume Muhammadi limegusiwa katika kazi yetu ijapokuwa halikuonyeshwa kwa mapana na marefu kwa sababu utenzi wetu umejikita sana hasa katika matukio ya vita vya kidini. Mtume Muhammadi ameangaziwa akituma miujiza ya uponyaji kwa Abdirrahmani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* hivyo basi suala la dini limetusaidia kuelewa zaidi uwezo wa Mungu kwa binadamu kupitia mtume wake.

Clark-Bekeleromo (1991) amezungumzia shujaa Ozidi Saga aliyetumia nguvu za kichawi pamoja na miti shamba kujikinga. Masimulizi kuhusu Ozidi Saga yanasawiri dini ya kuamini miungu, misimu na sihiri zingine. Kuamini huku pia kumejitokeza kupitia nguvu za miungu katika *Utenzi wa Abdirrahmani* na *Sufiyani.*

Hizi ndizo elementi za dini za asili zinazozungumziwa na Clark na ambazo zinahusiana na utenzi wetu isipokuwa mhusika Sufiyani hakutumia miti shamba wala sihiri katika imani yake bali aliongozwa na imani ya miungu katika matendo yake.

Swaleh (1992) amechambua maudhui katika *Utenzi wa Mwanakupona* hasa unaohusu kuwaasa wanawake wa Kiafrika kuwa na maadili kwa kusisitiza kuwa binadamu si lolote pasi Mungu. Mungu ndiye muumba wa dunia na vyote vilivyomo ndani, haya ni kwa mujibu wa dini ya Kiislamu. Utenzi huu unaleta uwiano wa suala la dini katika utenzi wetu kwani Mungu amepewa kipau mbele katika kutawala maisha ya binadamu, tofauti za tenzi hizi ni kuwa *Utenzi wa Mwanakupona* unazungumzia suala la maadili na *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* unazungumzia vita, usaliti na dhuluma miongoni mwa wahusika. Kipengee hiki cha maadili kimetufaa katika kufahamu dini kama chombo kinachoweza kubadilisha hulka mbaya za binadamu kuwa nzuri.

M'ngaruthi (2008) ameangazia vipengele vya fani kwa kugusia mtindo na maudhui, ploti, wahusika, dhamira, usimulizi, vichekesho pamoja na aina zingine za ngano. Kazi hii imetufaa kwa kiasi kidogo pale ambapo kipengee cha maudhui kimegusiwa sawia na utafiti wetu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.*

Watuha (2011) ameshughulikia maudhui ya Waadhi katika *Utenzi wa Adili* uliotungwa na Shabaan Robert. Kazi hii imesawiriana na mada yetu kwani tumechambua maudhui katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* hivyo basi tumepata mwelekeo mzuri wa kazi yetu. Uchambuzi wa maudhui hugusia masuala yote yanayohusu binadamu na mazingira yake katika shughuli zake zote za kila siku. Kwa upande mwingine, utenzi wetu hauna uwiano na *Utenzi wa Adili* kwa masuala kama vile: vita, ukafiri, usaliti na dhuluma n.k.

Ndumbu (2013) katika tasnifu yake ya uzamili amezungumzia matumizi ya takriri na sitiari katika U*tenzi wa Rasi 'lGhuli* unaohusu dini ya Kiislamu hasa katika harakati za kuanzishwa kwake Arabuni na jinsi vita vilizuka kutokana na uasisi wake ingawaje suala letu halina mshikamano wa moja kwa moja, tunapata tu upeo mdogo wa kurejelea kuhusu dini pale ambapo dini ya Kiislamu inahusishwa.

Owallah (2013) ametafiti uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Issa* dini ikiwa kati ya maudhui yanayoelezwa sawia na utenzi wetu unaomulika suala la dini hivyo basi tumeweza kuchota baadhi za elementi zinazohusiana na mada yetu kwa mfano nabii Issa kuzaliwa kwa njia ya miujiza na sifa za majagina kama vile ilivyo katika mhusika Abdirrahmani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Tofauti iliopo kati ya utenzi huu na wetu ni kuwa ushujaa wa Nabii Issa ulitumiwa kuendeleza maadili ilhali ushujaa wa Abdirrahmani uliendeleza maovu.

Vutagwa (2013) ameshughulikia *Utenzi wa Mwana Fatuma* katika tasnifu yake kwa kuangazia suala la dini pamoja na matukio ya kiajabu yanayopatikana ndani yake. Alionyesha jinsi arusi ilivyoandaliwa peponi hii ikionyesha tukio la ajabu sawia na utenzi wetu unaohusu pia ndoa ijapokuwa *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* una maudhui ya maovu tofauti na *Utenzi wa Mwana Fatuma.*

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Katika mbinu za utafiti tumeshughukilia njia zote ambazo zimetumika kuonyesha au kutambua data pamoja na zile zimetumika kutathmini matokeo ya utafiti. Tumeigawa sehemu hii.katika vijimada vitatu:

### 1.8.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Tumetumia sampuli ya kimakusudi kama mbinu ya kuteua sampuli yetu. Utafiti wetu umejihusisha na maktaba kwa kusoma kazi zingine zinazohusu maudhui. Kazi hizi ni kama vile: tasnifu zilizoshughulikia tenzi, riwaya na tamthilia husika. Tumeusoma na kuuelewa *Utenzi wa Abdirrahmani* na *Sufiyani* kwa kina pamoja na tasnifu zilizochanganua tenzi zinazozungumzia masuala mbalimbali ambayo yana uyakinifu wa maisha ili kupata uelewa zaidi kuhusu mada yetu. Mifano ya masuala haya yanayozingira maisha ya binadamu ni kama vile dini, ndoa,, maadili, vita n.k.

### 1.8.2 Ukusanyaji Data na Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu ambazo tumezitumia katika ukusanyaji data ni kama vile: kusoma na kuuchambua kwa kina utenzi tuliouchagua, kudurusu kazi mbalimbali maktabani zinazohusiana na uchambuzi wetu, kupitia tasnifu mbalimbali za wahakiki, makala yaliyoandikwa na waandishi tofauti tofauti yenye umuhimu katika utafiti wetu, vitabu na maelezo kutoka kwa mtandao (tovuti).

### 1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Baada ya kusoma kwa kina utenzi tulioushughulikia, tumechanganua na kutathmini data tuliyokusanya kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa kuonyesha thibitisho mwafaka kutoka kwa kazi husika na mwishowe matokeo ya uchanganuzi wetu tumeyawasilisha kwa njia ya maelezo na ufafanuzi.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeeleza utangulizi wa *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwa kutoa muhtasari mfupi kuhusu historia yake pamoja na thibitisho la kuonyesha asili ya utenzi wenyewe. Vilevile tumegusia maelezo mafupi kuhusu utafiti wetu wa maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya kinadharia, mihimili ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu fasihi, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu ya utafiti, mbinu za uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data na mbinu za ukusanyaji data na mwisho uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Vipengele hivi vyote ndivyo vimejenga sura ya kwanza ya kazi yetu ya uchanganuzi wa maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*.

# SURA YA PILI

## VIAMBAJENGO VYA MAUDHUI

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu viambajengo vinavyojenga na kuendeleleza maudhui. Viambajengo hivi ndivyo huonyesha uhusiano na mwingiliano wa mihimili ijengayo maudhui katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Maudhui ni jumla ya masuala yanayojitokeza katika kazi yoyote ile ya fasihi. Mawazo haya yote yanayozungumziwa katika fasihi hujumlisha vipengele vya mtindo na kwa hivyo maudhui hujengwa na mtindo ambao una vipengele vyake vya kimsingi ambavyo huchangia pakubwa katika kuleta uhusiano au mwingiliano wa karibu baina ya maudhui na mtindo katika utungo wowote ule wa kifasihi.

Gatakaa (2012) katika tasnifu yake ya uzamili anasema kwamba maudhui ni mawazo muhimu yanayoelezwa katika hadithi katika kazi ya fasihi na ambayo ni kioo cha jamii. Kutokaña na mawazo hayo ya Gatakaa, jamii halisi huelezwa kupitia kazi ya fasihi yenye wahusika anuai wakiwakilisha binadamu katika uyakinifu wao wa kimaisha. Vilevile Njogu na Chimerah (1999) wameeleza dhana ya maudhui kama mawazo ya mwandishi kwa mtazamo wa muktadha fulani.

### 2.1 Dhana ya Mtindo

Mtindo ni kipengele cha usanii kinachotumika kuwasilisha maudhui. Vipengele hivi ni kama vile wahusika, mandhari, msuko, usimulizi na fani kama vile chuku, balagha taswira n.k. Mtindo hujenga na kuendeleleza maudhui kwani matukio yote katika kazi ya fasihi hubainishwa wazi na vipengele hivi. Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa migogoro na matendo ya wahusika ndio huendeleza kazi ya fasihi.

#### 2.1.1 Wahusika

Wahusika ni viumbe vinavyowakilisha watendaji halisi katika maisha ya wanajamii. Viumbe hawa huwa ni viumbe hai na viumbe visivyo hai na ambavyo hudhihirisha wasifu wa ndani na nje wa wahusika lengwa kwa kuonyesha hali zao kama vile hali ya kusononeka au hali ya kufurahi kwa mhusika. Wahusika huonyesha uyakinifu wa maisha ambayo jamii huishi katika sehemu mbalimbali kama vile kazini.

Vilevile wahusika ni viumbe vya fasihi wanaoumbwa au kubuniwa na mwandishi kuwa sauti yake ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Wahusika hawa katika kazi ya fasihi huweza kuwa watu, wanyama, wadudu, mimea mazimwi, miungu, malaika na kadhalika. Kuna wahusika wakuu, wahusika wadogo na wahusika wasaidizi katika utunzi wa kazi yoyote ile ya kifasihi.Wahusika wakuu ni wale wanaowakilisha vitushi muhimu katika utungo fulani wa kifasihi. Wahusika wakuu hawawezi kutengwa na kazi ya fasihi kwani bila wao msuko wa vitushi hautakamilika.

Wamitila (2008) anasema kuwa wahusika huwa ni vielelezo vya jamii halisi ulimwenguni ingawa wahakiki wa fasihi wanakubaliana kuwa sifa zote za wahusika hazifungamani moja kwa moja na sifa za wahusika halisi au wanadamu husika katika mazingira yao halisi. Maudhui hujengwa na wahusika kwa namna ya kipekee kwani husawiri hulka zao ambazo huendeleza maudhui fulani. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umesawiri wahusika wengi mno kama vile Abdirrahmani, Sufiyani, Abubakari,Ayesha, mtume Muhammadi, Mora, Shamti bin Khadafu, Mikidadi, mkewe Abubakari, binti Sufiyani, Kinana, Kaaba, Shamlani, malaika wa Mungu, majeshi wa upande wa Abdirrahmani na Sufiyani pamoja na wahusika wengine wengi katika hadithi hii.

Wahusika wanaweza kuwa wakuu, wadogo au wasaidizi katika kazi ya fasihi. Wahusika wakuu ni wale wanaozingirwa na mambo yote yanayotendeka kwenye hadithi kuanzia mwanzo wa kisa hadi kilele chake hivyo basi wanajenga maudhui makuu. Wahusika wadogo hawana nyadhifa kuu katika kuendeleza maudhui mazito katika kazi ya fasihi husika nao wahusika wasaidizi hukamilisha tu maudhui katika kisa; kwa hivyo utungo wowote ule unaweza kukamilishwa pasi na mchango wa wahusika wasaidizi. Wahusika wakuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ni Abdirrahmani, Sufiyani na mtume Muhammadi. Wahusika wale wengine wanachukuwa nyadhifa za wahusika wadogo na wahusika wasaidizi. Abdirrahmani kama mhusika nguli anaonyesha sifa za ushujaa vitani kwa hivyo anaendeleza maudhui ya ushujaa/ ubabe katika hadithi nzima.

Senkoro (2011:7) anasema kuwa wahusika ni watu au viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi ya fasihi. Tunakubaliana na mawazo yake kuwa wahusika ni viumbe wanaobuniwa na mtunzi ili kuwasilisha binadamu katika hali yao halisi ya maisha.

Mtunzi hutumia wahusika hao katika kujenga na kuendeleza ujumbe wake kupitia yale wanayotenda kwa mfano mhusika kama vile Sufiyani ambaye ni nguli, ametumiwa na mtunzi kuonyesha sifa ya kuwa katili ili kuendeleza maudhui ya ukatili katika kazi hii.

*Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umesawiri wahusika mbalimbali ambao wana sifa mbalimbali zinazowakilisha watu katika jamii. Kuna aina mbili za wahusika kulingana na Gatakaa (2012): wahusika nguli na wahusika hasidi. Mhusika nguli ni yule anayekuwa na sifa za ujasiri za kuweza kukabiliana na jambo lolote lile bila woga na zaidi ya hayo hupigania kutetea haki zake kutokana na pingamizi za wahusika hasidi katika jamii anamoishi. Abdirrahmani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ni mfano wa mhusika nguli anayepigania haki zake dhidi ya mpinzani wake Sufiyani. Mhusika hasidi katika hadithi ni yule hafurahishwi na mafanikio ya wahusika wengine. Analeta mkinzano na mvutano katika harakati za kumzuia mhusika nguli kuafikia malengo yake ya maisha kulingana na uteuzi wake wa moyoni. Sufiyani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ni mhusika hasidi kwani anakuwa pingamizi kwa juhudi za Abdirrahmani za kutaka kuridhiana na jamii yake. Vilevile Sufiyani anapinga jitihada za bintiye za kutaka kwenda na mumewe Madina. Mtume Muhammadi pia ni mhusika nguli kwani anadhihirisha ujasiri wa kuwa na uwezo wa kutenda miujiza kwa waumini wake.

Wamitila (2003:123) anasema kwamba mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya fasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wahusika huwakilisha mawazo ya mtunzi katika kuafikia shabaha yake kwa hivyo wahusika wana majukumu ya kuendeleza kazi ya fasihi. Tumekubaliana na mawazo haya kwani wahusika wanaowakilisha kazi ya fasihi huwa na sifa za kibinadamu za kutenda vitendo fulani ili waweze kuwa kioo cha jamii.Shamti bin Khadafu ni mhusika ambaye ni kielelezo cha watu katika jamii wanaopitia changamoto za maisha kutokana imani yao katika dini.

Vilevile wahusika hutambulishwa na msimulizi au wahusika wenzao katika kazi yoyote ile ya fasihi. Hulka za wahusika zinazosawiri maadili fulani zimebainika wazi katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* hasa kwa mhusika Abubakari ambaye anahuzunishwa na maovu ya mwanawe ndiposa anajishughulisha kumsihii arudie dini

ya kweli kwani ndio hujenga maadili. Abubakari ni kielelezo cha watu wenye hekima katika jamii wanaoweza kushawishi watu wenye tabia hasi na kuwa watu wema kama alivyomshauri Abdirrahmani kuacha ukatili wake.

### 2.1.2 Mandhari

Mandhari katika kazi ya fasihi hutumika kujenga na kuendeleza maudhui. Mandhari ni mahali ama wakati tukio la kifasihi lilipobuniwa na mwandishi na huwa ni mazingira ya utendaji au usimulizi. Msomaji huweza kujua ni wapi na lini matukio fulani yaliyowasilishwa yalifanyika hivyo basi mandhari ni elementi muhimu katika usimulizi wowote ule wa kazi ya fasihi. Wataalamu mbalimbali wameeleza dhana hii ya mandhari kwa mtazamo tofautitofauti na miongoni mwao ni Mbatiah (2001) na Wamitila (2008).

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa mandhari ni mahali maalum ambapo msanii alijenga ili wahusika waweze kukaa na kuingiliana katika kuzua matukio ya kiutendaji. Tunapata uelewa wa mandhari kutokana na maelezo haya kuwa ni pale ambapo wahusika hufanyia vitendo vyao au mazingira maalum ambayo wahusika huwa wanapokuwa wakitenda vitendo fulani katika uigizi au usimulizi wowote ule katika kazi ya fasihi. Msomaji hupata taswira halisi ya matukio kupitia ubunifu mzuri wa mandhari ndiposa mandhari ni mhimili muhimu katika ujenzi wa maudhui kwani pasi mazingira ya masimulizi au uigizaji msomaji hawezi kuelewa na kufuatilia ni wapi na ni lini matukio fulani yalitendeka.

Mbatiah (2001:42) anasema kuwa mandhari ni istilahi inayohusishwa hasa na utanzu wa drama. Kulingana na maelezo haya, mandhari ni sura itokanayo na urembo wa jukwaa ambayo imekusudiwa kuiga mazingira ya jamii halisi wanamoishi kama vile kazini, nyumbani au hata uwanja wa vita kama ilivyo katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ambapo mwandishi amesawiri jinsi vita vinavyofanyika nyikani (ubeti 579). Wamitila (2004) anakubaliana na maelezo ya Mbatiah kwa kusema kuwa mandhari huhusisha mazingira ya jukwaa pamoja na wakati ambao matukio yanatendeka. Maelezo haya yanarejelea mazingira na wakati wa matukio kama vipengele muhimu vinavyofungamana katika kujenga mandhari.

Tunakubaliana na Wamitila (2008) anaposema kuwa mandhari ni mazingira ya kimahali, kiwakati na ya kihistoria ambayo kazi ya fasihi inajijenga. Mandhari ni kipengele cha kimsingi ambacho kinajenga maudhui kwani matukio yote yanayoelezwa katika kisa fulani lazima yawe yanatendeka mahali maalum na pia kwa wakati fulani kwa hivyo mtunzi huteua mandhari yake mwenyewe kulingana na ujumbe anaonuia kuupitisha kwa hadhira. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ulitungwa katika kipindi cha utasa katika historia ya ushairi. Kipindi hiki ndicho maandishi ya fasihi kwa jumla yalikuwa machache na kwa hivyo pia maudhui hayakuwa mengi. Maudhui katika enzi hizo yalilenga kuadilisha jamii hasa dini ikiwa kipengee cha msingi.

Kuna migao mitatu ya mazingira katika mhimili huu wa mandhari: mgao wa eneo halisi la kijiografia, mgao wa amali ya wahusika na desturi zao za maisha yao ya kila siku na mgao wa wakati ambapo tukio fulani limetendeka pamoja na kipindi maalum katika historia. Mgao wa eneo halisi la kijiografia ni mazingira kama vile chumba cha nabii panapofanyika maombi au sala. Mhusika Shamti bin Khadafu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* anakwenda kwa nabii kutafuta faraja kutokana na dhuluma anayopitia kutoka kwa Abdirrahmani (ubeti 71).

Vilevile Mandhari ya kijiografia hubadilika kulingana na maudhui yanayolengwa kwa mfano *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umeonyesha mandhari tofautitofauti kama vile msikitini na ambayo maudhui ya dini yanajitokeza na pia mandhari ya uwanjani yanadhihirisha matukio ya vita yanayowakumba mashujaa katika safari zao. Hadithi hii imesimuliwa kutoka bara la Asia, nchi ya Saudia, mji mkuu wa Riyadh na mahali husika ikiwa ni Madina. Mandhari haya yanadhihirisha wazi kuwa matukio katika kisa hiki yalitendeka panapojulikana.

Mgao wa pili ni wa amali za wahusika na desturi za maisha yao ya kila siku. Huu mgao wa pili unaonyesha imani na itikadi za wahusika katika maisha yao kwa mfano mhusika Shamti bin Khadafu anaacha mali yake yote na kwenda kutafuta imani ya dini ya Kiislamu baada kugundua kwamba maisha bila mwongozo wa 'Allah' yalikuwa bure licha ya kutunukiwa na ukwasi (ubeti 47). Mgao wa tatu ambao ni wa wakati ambapo tukio limetendeka katika kipindi maalum katika historia.

*Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umejikita katika kipindi ambacho dini ya Kiislamu ilikuwa inapata maenezi yake na kupitia pingamizi kutoka kwa wahusika wasioamini Mungu hivyo basi kuzua mandhari yanayosawiri maudhui ya usaliti na dhuluma.

### 2.1.3 Msuko

Msuko unarejelea mfuatano au mpangilio maalum katika kazi ya fasihi. Mpangilio huu pia huitwa ploti. Mbatiah (2010) anelezea msuko au ploti kama mfuatano wa matukio na ubainishaji wa asili yao. Tunachanganua mawazo ya Mbatiah kuhusu msuko kwa kusema kuwa msingi mkuu wa ploti ni matendo ya wahusika ambayo yana mpangilio maalum kuanzia mwanzo, kati na mwisho. Sehemu ya mwanzo husawiri mwanzo wa mgogoro unaomhusu mhusika nguli katika hadithi yaani matukio yake yanapoanza yanasawiriwa kwa hivyo msomaji hutegemea sehemu hii ili aweze kuwa na hamu ya kuendelea kusoma hadithi nzima. Kisa katika utenzi wetu kimeanza kwa taharuki pale ambapo mtunzi anasema kuwa aliadithiwa na babu yake na kwa hivyo ana ujumbe kamili kuhusa shujaa Abdirrahmani. Vilevile utangulizi wake unaonyesha maenezi ya dini ya Kiislamu na jinsi mhusika Shamti bin Khadafu alivyojitolea kufuata Uislamu hivyo basi msomaji anapata hamu ya kutaka kujua yaliyotendeka baada ya usimulizi huu. Sehemu ya kati huonyesha maendelezo ya matendo na namna yanavyokuza mgogoro unaomhusu mhusika nguli katika hadithi. Maendelezo ya matukio ya mhusika nguli yaani Abdirrahmani yanasawiri hulka zake mbaya dhidi ya wahusika wengine katika hadithi. Mwisho, sehemu ya tatu inahusu kilele cha migogoro katika hadithi na ambayo kusuluhishwa kwake kunaafikiwa. Hadithi hii inafikia mwisho wake, vita vya kidini vikileta maridhiano miongoni mwa wahusika. Msomaji anaweza kutathmini usomaji wake baada ya kusoma matukio haya kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Msuko kwa maelezo mengine ni muundo wa hadithi katika kazi ya fasihi. Wahakiki wengine wa kazi za fasihi wamefasiri muundo kama mpangilio wa matukio katika utungo fulani wa kifasihi ambao huleta mtiririko wa masuala yanayoelezwa (maudhui) kwenye kisa. Muundo unaweza kuwa sahili au changamano. Ploti ya vitushi katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ni sahili kwani matukio katika hadithi yamefuatana kama yalivyotendeka kutoka mwanzo hadi mwisho hivyo basi msomaji hupata nafasi ya kuelewa kisa hiki bila kuchanganyikiwa.

Wamitila (2003) anaelezea aina za misuko katika kazi ya fasihi kama vile: msuko kinzani, msuko msago, msuko mkuu, msuko kioo na msuko rudufu. Msuko msago au msuko sahili umejitokeza katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Matukio yanahadithiwa kwa njia ya moja kwa moja kuanzia mwanzo hadi mwisho vitushi hivyo vikijikita katika wahusika nguli ambao ni Abdirrahman na Sufiyani hivyo kumpa msomaji mnato au mvuto wa kipekee wa kusoma hadithi hiyo bila kuchanganyikiwa au kukata tamaa ya kuendelea kusoma.

### 2.1.4 Sauti ya Usimulizi

Sauti ya usimulizi ni mbinu ambayo mwandishi hutumia kusimulia hadithi yake. Wataalamu mbalimbali wamegusia suala hili la usimulizi kwa mitazamo mbalimbali. Madumulla (2009:110) anasema kwamba "usimuliaji ni mbinu katika fasihi inayobainisha sehemu alipo anayesimulia hadithi au tukio". Maelezo haya yanarejelea picha inayojengeka akilini mwa msomaji kutokana na usimulizi wa hadithi. Msomaji hupata taswira kamili ya matukio na jinsi matukio hayo yanavyohusiana, yanavyoingiliana na yanavyoendelea kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Njogu na Chimerah (1999) wanafasiri usimulizi kama sauti ya uwasilishaji wa kisa au hadithi. Wanaeleza zaidi kuwa kuna aina mbili za usimulizi ambazo mtunzi hutumia katika kazi yake kama vile: usimulizi wa nafsi ya tatu na usimulizi ambapo mhusika mmoja kati ya wahusika wengine anasimulia hadithi. Usimulizi huchangia pakubwa katika umaizi wa kazi ya fasihi kwani humuelekeza msomaji katika kufuatilia matukio hadithini bila kupotoka. Kulingana na Wamitila (2008) watunzi wengi wa kazi bunifu huzoea kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza na ya tatu hata hivyo kuna utumizi finyu wa nafsi ya pili katika kazi ya fasihi kwa jumla isipokuwa kazi chache zilizoshuhudiwa kutumia nafsi ya pili. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umechanganya usimulizi wake katika nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Hadithi hii imejikita katika aina hizi za usimulizi kwani imepokezanwa kutoka kwa msimulizi mmoja hadi kwa mwingine. Matumizi ya nafsi ya kwanza yanajitokeza pale ambapo mhusika Shamti anamweleza nabii Muhammadi jinsi alivyoamua kufuata dini ya kweli kwa kusema "Nilipokwisha shahidia..." ( ub. 47). Sufiyani anakata kukiri Uislamu kwa kusema " Niua hima nondoke..." (ub. 954).

Vilevile matumizi ya nafsi ya tatu yanajitokeza pale ambapo mhusika Mora anamweleza Abdirrahmani mpango wake wa kutaka mtume Muhammadi kuwaauni vitani kwa kusema "Akamwambia ni kheri ulilofanya shauri..." (ub. 584). Sufiyani alipokataa kukiri Uislamu, nabii anamwagizia Sheikh Ali amuue kwa kusema "Akatamka Rasuli... (ub.659).

Msuko mzuri wa vitushi ndio humpelekea msomaji kuwa na ukakamavu wa kusoma na kuelewa kisa fulani hivyo kufanikisha malengo ya mwandishi kwa hadhira. Uelewa wetu kuhusu usimulizi ni kuwa unaweza kuangaziwa kwa mitazamo miwili: mtazamo wa ndani na wa nje. Mtazamo wa ndani huangazia msimulizi akishiriki katika hadithi kama mhusika na ambapo inayosimulia huwa ni nafsi ya kwanza. Mtazamo wa nje katika usimulizi hautambuliki wazi lakini nafsi ya tatu ndiohuwakilisha, kiambishi 'a' kikitambulisha usimulizi huu. Msimulizi huweza kupatikana kila mahali kwa wakati mmoja na kufahamu matukio yote yanayojiri kuanzia mwanzo hadi mwisho. Maoni haya Wamitila (2008) yametuelekeza hasa katika kuchunguza nafsineni katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.*

Wahakiki wa fasihi wameweza kutumia usimulizi kwa njia tatu katika kazi zao: usimulizi wa nafsi ya kwanza,ya pili na tatu. Usimulizi wa nafsi ya kwanza huchukua mtazamo wa ndani ambapo mhusika mmoja ana nyadhifa mbalimbali katika hadithi kama vile kutazama na kutathmini matukio. Usimulizi huu hutambulishwa na kiwakilishi 'mimi' au mofu 'ni' katika kitenzi husika. Mhusika katika usimulizi wa nafsi ya kwanza hueleza yale anayoyashuhudia au anayoyapitia. Usimulizi wa nafsi ya pili huchukua kiwakilishi 'wewe' au mofu 'u' na si usimulizi wa kawaida katika sanaa ya uandishi, nafsi ya tatu nayo huchukuwa kiwakilishi 'yeye' au mofu 'a' na ndio hutumiwa sana katika tanzu zote za fasihi kama vile riwaya na ushairi. Hadithi katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* imebainisha matumizi ya nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu kwani kisa kinaelezwa na mhusika anayepitia jambo fulani na kwa upande mwingine, mhusika mwingine anaeleza jambo hilo ambalo mhusika huyo analipitia. Mfano mwafaka kutoka kwenye utenzi, ni pale ambapo nabii anamtuma Sheikh Ali kumuua Sufiyani kwa kusema "Akenda hima imamu..." (ub. 964) na pia anamwambia Amini aende kumuauni Abdirrahmani vitani kwa kusema "Akamwambia Amini..."(ub. 849).

## 2.2 Hitimisho

Katika kuhitimisha sura hii ya pili, tumejadili viambajengo vya maudhui kwa kueleza jinsi vinavyojenga na kuendeleza maudhui katika kazi yetu. Tumeeleza mtindo kama mhimili wa kujenga maudhui na ambao una vipengele vyake vya kimsingi vinavyosaidia katika ujenzi huu wa maudhui. Vipengee hivi ni kama vifuatavyo: wahusika, mandhari, msuko, sauti ya usimulizi na fani. Mawazo ya wahakiki mbalimbali waliochangia katika dhana hii ya maudhui na mtindo yameangaziwa katika sura hii kwani maoni yao yametufaa katika kuchanganua kazi yetu ya maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Tumetoa baadhi ya mifano ya beti kutoka kwenye utenzi wetu kama thibitisho la kuupa nguvu uchambuzi wetu wa maudhuimbalimbali.

Wahusika katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* wamechangia pakubwa katika kujenga na kuendeleza maudhui haya makuu kwa sababu katika kila suala, lazima kuwe na mtendaji anayehusishwa na matendo fulani. Kuna wahusika walioweza kupata mafanikio ya maisha baada ya vitushi vyote katika hadithi na vilevile kuna wale hawakuweza kupata mafanikio au ushindi hivyo basi kuangamia au kupelekea kufanya uamuzi fulani bila hiari yao na ndio maana imetubidi kushughulikia jinsi maudhui haya makuu yanaleta uhalisia au uyakinifu katika jamii ya sasa katika sura ya nne. Maudhui makuu katika utenzi wetu yameaangaziwa katika sura ya itakayofuata (sura ya tatu) na tumechambua maudhui kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.*

# SURA YA TATU

## MAUDHUI MAKUU KATIKA UTENZI WA ABDIRRAHMANI NA SUFIYANI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii ni muhimu mno katika utafiti wetu, kwani ndio kiini cha uchambuzi wetu wa maudhui. Uchambuzi huu wa kimaudhui katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ulituelekeza katika kufahamu zaidi viambajengo vinavyohusiana na mada hii ya maudhui hivyo basi tuliweza kuangazia viambajengo hivyo kwa kifupi, ili kuleta uelewa wa dhana ya maudhui kabla ya kuanza kuchambua maudhui yenyewe. Fasili mbalimbali zimetolewa na wahakiki wa fasihi kuhusu maudhui. Mbatiah (2010) anaeleza kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Maelezo ya wasanii wengi tuliowataja kuwa walichangia katika kugusia suala hili la maudhui wameafikiana na kushabihiana na fasili ya Mbatiah.

Tumechanganua maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. 'Makuu' ikiwa maana ya kuchagua kitu au jambo lenye uzito kati ya vitu vingine au mambo mengine yanayozungumziwa kwenye matini fulani. Hii ina maana kuwa, kuna maudhui mengi katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*, lakini tumechagua tu yale yenye uzito na ambayo yanaweza kubeba maudhui madogo madogo yaliyosalia, hivyo basi maudhui haya madogo madogo hupatikana ndani ya maudhui makuu ili kuongeza uzito wa maelezo.

### 3.1 Dini

Dini ni imani katika kuwepo kwa Mungu au kiumbe mwenye nguvu zaidi ya binadamu. Dini huwa ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho na kwamba kuna Mungu ambaye aliumba ulimwengu huu na ndiye mtawala wa kila kilichomo. Wanaongeza zaidi kwa kusema kuwa ni mfumo fulani wa imani hii na njia ya kuabudu, kusali na kuheshimu / kutii huyo muumba kama wafanyavyo Wakristo, Waislamu na waumini wengine duniani. Tunaafikiana na maelezo haya na kupata maana ya kijumla kuwa dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho na ambayo humwongoza binadamu katika kutenda mabaya au mazuri ulimwenguni kulingana na imani anayoshikilia.

Dini ya Kiislamu imerejelewa katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* hivyo basi matendo yanayofanywa na binadamu yamehusishwa na mwongozo wa 'Allah' na nabii wake Muhammadi.

Mwandishi wa *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* amesawiri nguvu za dini kwa namna mbalimbali hasa katika kutenda miujiza na mambo yanayomwongoza binadamu. Ameangazia dini ya Kiislamu kwa mapana na marefu kwa kuonyesha nguvu zinazompa Mungu uwezo mkubwa dhidi ya nguvu hafifu za miungu. Ulinganisho wa Mungu na miungu umesawiriwa katika imani ya wahusika katika kisa. Maudhui ya dini yameangaziwa na wahusika katika utenzi wakishikilia Uislamu na ukafiri. Pia dhana ya dini ndio imebeba maudhui madogo madogo kama vile miujiza, maadili na mabadiliko katika dini miongoni mwa wahusika katika hadithi.

### 3.1.0 Uislamu na Ukafiri

Uislamu ni imani katika dini inayoamini na kushikilia kuwa kuna Mungu mmoja anayepaswa kuabudiwa na aliyeumba mbingu na ardhi na kuwa na mtume wake wa mwisho Muhammadi ilhali ukafiri ni imani ya kutoamini dini ya Kiislamu hasa kwa kutenda mambo yanayoenda kinyume na sheria au ibada zao za Uislamu.

Mdee *nw* (2011), wanasema kwamba Uislamu ni dini ambayo msingi wake ni Kurani Takatifu na ambayo inashikilia kuwa Mungu anayestahili kuabudiwa ni mmoja tu na kwamba mtume wake Muhammadi ndiye mjumbe wake wa mwisho. Dini ya Kiislamu hufuata imani ya kuwepo kwa Mungu mmoja anayepaswa kuabudiwa na mtume wake Muhammadi. Maelezo haya kuhusu dini yanatuelekeza katika kuelewa zaidi maana ya dini ya Kiislamu na kulingana na umaizi wetu tunakubaliana na mawazo yao kwa kusema kuwa dini ya Kiislamu huamini uwepo wa Mungu mmoja (Allah) na ambaye mjumbe wake wa mwisho ni Muhammadi.

### 3.1.1 Uislamu

Dini ya Kiislamu imejitokeza bayana katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*, kwani umeonyesha wazi kwamba Mungu ndiye mwenye kuabudiwa na hakuna Mungu mwingine. Mwandishi ametanguliza hadithi au historia yake kwa kumsifu Mungu mwenye wingi wa rehema (Ar- Rahman) anayestahili kuabudiwa pekee.

Mtunzi anaendelea kumsifu Mola zaidi kwa kusema kuwa ni mwenye uwezo juu ya kila kitu kwani ndiye mmiliki wa kila kitu kilichomo ulimwengu (Al- Muqtadir). Muhammadi ndiye mtume wake Mola mpendwa aliyemuumba (ub. 1-3).

Dini ya Kiislamu ina majina tisini na tisa ya kumtajia na kumsifu Mungu na majina haya yote yanampa uwezo juu ya binadamu na vyote vilivyomo duniani na akhera. Baadhi ya sifa za Mungu zimetajwa katika utenzi wetu hasa katika utangulizi wa hadithi. Mtunzi ameanza kwa kueleza kisa chake kwa kusema, anaanza kwa jina la Mungu mwenye rehema kwani ndiye anayerehemu waja wake.

Bismillahi nandike
'rRhamani yu pweke
Rahimu zote zi kwake
wajawe hutuletea (ubeti1)

Suala la imani limesisitizwa kwani ndio mwongozo wa maisha ya binadamu duniani. Binadamu anaelezwa kuwa atakayepuuza dini ataangamia. Kuangamia huku kulingana na dini ya Kiislamu, ni adhabu ya kwenda motoni na ambayo Mungu huitoa kwa wasiomuamini. Vilevile Mungu mmoja ndiye anayestahili kuabudiwa na hakuna kama yeye duniani na akhera. Dini ya Kiislamu imebainisha wazi msingi wa imani yake kuwa ni kuabudu Mungu mmoja pekee (ub. 2-3). Baadhi ya majina yanayotumiwa kumsifu Mungu ni kama vile: Al- Malik (mfalme wa milele), As-Salaam (mwenye kuleta amani), Al- Khalaq (muumbaji), Al- Ghaffar (mwenye kusamehe) n.k.

Shahada kama nguzo ya kwanza katika dini ya Kiislamu imebainika wazi kwa mhusika Shamti bin Khadafu. Mwito wa imani ya Uislamu ulimjia Mwarabu (Shamti bin Khadafu) na kumpa msukumo wa kuacha kila kitu alichokuwa nacho duniani, baada ya kung'amua kuwa maisha bila dini yalikuwa bure. Mwarabu aliacha ukwasi wake wote, hususan cheo kikubwa, mali nyingi yenye thamani pamoja na jamii yake waliomtegemea kwa kila jambo ili kusaka ukweli wa dini ya Kiislamu kutoka kwa nabii. Mwarabu anawahubiria jamaa zake kuhusu dini ya Kiislamu kisha wanakubali na kukiri imani hiyo bila pingamizi yoyote (ub. 47-48 na 50)

Nilipokwisha shahidi
hawakusanya junudi
wanangu na maabidi
nao kuja shahadia (ubeti 47)

Kuwepo kwa sehemu ya kuabudia kama vile msikiti ni ishara ya imani ya Uislamu pamoja na kiongozi wa dini. Mwarabu alipoamua kukiri imani ya Uislamu aliendamoja kwa moja hadi msikitini akijua dhahiri kuwa atampata nabii pale. Alifahamu kuwa usaidizi wake wa kiroho angeupata pale msikitini. Pia tunaelezewa kuwa siku ambayo Mwarabu alipofika msikitini kwa nabii, alimkuta nabii ameketi na waumini wengine wa dini ya Kiislamu hili likiwa thibitisho wazi kuwa msikiti ni ishara ya dini kwa hivyo shughuli zingine za imani ya Uislamu hufanyika mle (ub. 27, 30-31).

Sala kama nguzo ya pili katika imani ya Uislamu imedhihirika pale ambapo mkewe Abubakari aliposali kwa ajili ya safari ambayo mumewe alikuwa nayo ya kwenda kumuauni Abdirrahmani baada ya kuarifiwa na mtume kuwa alikuwa anawadhulumu watu kutoka nchi zote. Mkewe alimwombea mumewe kwa Mola amlinde dhidi ya simba njiani na katika hatari zozote ambazo zingeweza kutokea safarini. Maombi haya yanaashiria jinsi dini ilivyojikita katika familia hii ya Abubakari na kuonyesha namna wanavyoishi kwa njia ya uaminifu inayoongozwa na maadili yatokanayo kwa dini. Dini huadilisha jamii na kuwaelekeza katika njia ifaayo inayoleta amani miongoni mwa jamii (ub.93-95).

Niombea kwa mannani
leo nangia ndiani
kwa AbdurRahmani
ambako nakusudia (ubeti 95)

Dini ina uwezo wa kumshawishi mtu kuacha njia zake mbaya na kuwa mwema. Abubakari alimhubiria Mora hadi akakiri dini ya Kiislamu jambo ambalo ushawishi mkubwa ulitokana na mahubiri kuhusu imani hiyo ili Mora aweze kufahamu kwa kina dini. Ushawishi wa kumsilimisha Mora ulichangiwa pakubwa na ile hali ya Mora kuwa na mwelekeo chanya kuhusu Abubakari. Tumeelezewa kuwa Mora alikiri kwa kinywa chake mbele ya Abubakari kuwa alionekana mtu mzuri aliyeadilika kutokana na dini ya Kiislamu walipoonana kwa mara ya kwanza hivyo basi uhusiano huu ndio ulimfanya Mora kusilimishwa na Abubakari. Vilevile, Mora anamwambia Abubakari

kuwa anamwona kama mfuasi wa dini ya Kiislamu na anayempenda mtume Muhammadi (ub.107-108 na 120).

Falsafa ya dini ya Kiislamu hubainisha wazi kwa waumini wake kuwa, ulimwengu sio pahali pazuri kwani kuna mambo mengi yanayowadanganya hatimaye kuwatumbukiza jehanamu.Waraka aliouandika Abubakari kwa Abdirrahmani ulikuwa umejaa ushawishi wa dini wa kumrai mwanaye kumrudia Mungu na kuepuka adhabu ya kaburi, baada ya maisha ya hapa duniani. Abubakari anamkumbusha jinsi alivyomlea tangu utotoni kabla ya kupotea na kwenda kuabudu miungu. Maneno ya Abubakari kwenye waraka huo yalisheheni mawaidha kwa mwanawe hasa ya kumsihi kuachana na mambo ya ulimwengu yanayomdanganya aingie motoni. Vilevile, wanamweleza kuwa amhofu Mungu pekee kwani neno lake ndilo litamfaa (ub.156 na 157).

Mkhofu Mungu mwanangu
ghururi ya ulimwengu
yendemene na matungu
adhabu ya kaburi (ubeti 157)

Mtume Muhammadi anatimiza nguzo ya Uislamu ya kusali kwa minajili ya janga linalomkumba Mwarabu. Kuachiliwa kwa mwanaye Shamti bin Khadafu baada ya kutekwa nyara kulikuwa kwa kimiujiza kwani nabii Muhammadi alimhakikishia kuwa mwanake hangedhurika katika hali yoyote ile, licha ya kuwa amezuiliwa na Abdirrahmani ambaye ni katili. Alimwombea akiwa na imani ya kuwa Mungu pekee mwenye uwezo wa kutenda mambo yote atamnusuru na hatimaye ikawa kama alivyonena nabii. Nguvu za dini ya Kiislamu zinadhihirika wazi katika kuleta utulivu hasa kwa mhusika Shamti bin Khadafu aliyekuwa amesononeka kutokana na ukatili aliokumbana nao njiani akielekea Madina kwa nabii Muhammadi (ub. 67, 73 na 185).

Dini ya Kiislamu inajitokeza kwa mhusika Abdirrahmani alipokiri mbele ya Mora kuwa anatubu aliyoyafanya, kwani alimwacha babake na dini ya kweli na kumfuata Sufiyani mwenye dini ya uongo. Haya majuto yake yote yanatokana na kutusiwa na bwana mkuu wake, licha ya kumfanyia kazi kwa uaminifu. Pia kichocheo kingine ni waraka kutoka kwa babake, ambao ulikuwa na ujumbe wa kumtaka arudi nyumba hivyo basi akaamua kumuasi Sufiyani na miungu yake na kumrudia Mungu.

Abdirrahmani anang'amua kuwa alikuwa kwenye giza na maisha yake pia yalikuwa hatarini. Matendo yake Abdirrahmani ya kuenda kinyume na dini ya Kiislamu yanaonekana wazi baadaye alipowaza kuhusu maisha yake ya hapo awali alipokuwa akiamini Mungu, kwa kutofautisha faida anazozipata kutokana na imani hizi mbili. Ung'amuzi wake kuhusu dini ya kweli unampa uamuzi wa kushahidia tena dini ya Kiislamu aliyokuwa ameiasi na pia kuridhiana na wazazi wake.

> kuliko na baba yangu
> siwati dini ya Mungu
> hafuata uasi (ubeti 224)

Nguzo ya dini ya Kiislamu inadhihirishwa katika sala ya Abdirrahmani kwa Mola anayeweza yote ulimwenguni. Abdirrahmani analitaja jina la "Allah" pindi anapokwenda kukabiliana na Sufiyani mlimani. Anamwomba Mola asimwingize vitani baada ya kuona wanajeshi wengi wa Sufiyani tayari kumkabili. Dini inadhihirika hapa kwani Abdirrahmani anategemea nguvu za Mungu hasa katika vita anavyovipitia anaamini kuwa Mungu pekee ndiye anayeweza kuauni. Vilevile, dini ya Kiislamu inajitokeza pale ambapo Abdirrahmani alisifu jina la Mungu kama lenye uwezo wa kumwezesha mtu kupata pahali pazuri pa kukaa baada ya maisha ya ulimwengu kwa hivyo humpa binadamu matumaini ya kuishi vyema duniani na akhera ili kuepuka adhabu ya jehanamu (ub. 228).

Uwepo wa malaika wa Mungu pamoja na mtume Muhammadi ni ishara ya dini. Kulingana na dini ya Kiislamu, Mungu ana malaika wengi mno kwa mfano malaika Jibrili ana jukumu la kuleta ufunuo wa Koran kwa mtume Muhammadi. Malaika Jibrili anatumwa na Mungu kama mjumbe wake kwa Abdirrahmani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* ili kuleta mawasiliano ya kiroho kati Mungu na Abdirrahmani.

> Enzi ni yake Jallahi
> na dini yake rasuli
> kesho nipate jevuli
> mahali pa kwenda kaa (ubeti 345)

Suala la dini linajitokeza pale ambapo Abdirrahmani na Mora wanatimiza nguzo ya kwanza ya Uislamu ya kuamini Mungu pekee kama mwenye uwezo mkubwa wa

kutenda mambo makuu kwa binadamu. Abdirrahmani anajeruhiwa vitani kisha anakiri imani yake kwa Mungu na mtume wake Muhammadi. Kukiri kwake kwa imani hii kulionyesha hali ya kufika mwisho wa kutegemea nguvu zake za mwili na kutegemea za Mungu pekee. Vilevile, Mora anashuhudia idadi ya wanajeshi wa Sufiyani wakiongezeka vitani kisha anamuarifu Abdirrahmani lakini badala yake hatishiki bali anamjibu Mora kuwa lazima Mungu amemtuma malaika wake Jibrili kwa Muhammadi ili kuleta msaada wake hivyo basi haoni haja ya kubabaika ( ub. 415-416 na 436).

Kulingana na dini ya Kiislamu, mtu huwezakuomba dua kwa Mungu kulingana na mahitaji yake. Mkewe Abubakari anamwombea dua mumewe kwa Mungu anapoenda safari ya mbali ili Mola amkinge dhidi ya hatari njiani. Binti Sufiyani anamwombea mumewe apone baada ya kujeruhiwa vitani ili aweze kurudi kupigana. Hali hii inaonyesha imani yao kwa Mungu hasa katika dua waliyoiomba iliyosheheni matumaini yake yote yakitegemea Mola. Suala hili la dini limeonyesha wazi kuwa binadamu hutegemea Mungu anapokumbwa na majanga fulani hasa yanayomshinda kujinasua (ub. 451).

Kuumia kwa Abdirrahmani kuliwaacha wote bila matumaini ndiposa walibakia kumuomba Mola kutuma msaada kwani vita havikuwa vimefika mwisho kwa hivyo walingoja kwa hamu miujiza kutendeka juu yao. Abdirrahmani anapata usaidizi kutoka kwa majeshi waliotumwa na nabii kwa sababu ya imani yake katika Uislamu ambayo ameishahidia kuabudu Mungu pekee na mtume wake Muhammadi (ub. 493,495,504 na 516).

Miujiza ambayo Mungu alimtendea Abdirrahmani ilikuwa suala linalohusiana na imani. Abdirrahmani alipata uponyaji wa moja kwa moja kutoka Mola aliyemtuma Sheikh Ali kupitia nabii baada ya kumgusa tu na vidonda alivyokuwa navyo vilipona papo hapo na kisha akaamka na kumshukuru Mungu. Miujiza kama hii hutendeka panapokuwa na imani thabiti na hivyo Abdirrahmani anapona kutokana na imani yake kwa Mungu (ub. 622-623).

Miujiza yote kwenye utenzi imeletwa na uwepo wa imani katika dini ya Kiislamu. Nabii anaonyesha ushujaa wake kwa binadamu kutokana na suala la dini kwani

amepewa uwezo na Mungu wa kufanya miujiza kama vile kumponya Abdirrahmani papo kwa hapo alipoumia vitani, kuwapa nguvu za kimiujiza wanajeshi wake walipokwenda vita kwa mfano kutumia mchanga kuwaua wapinzani wao. Mambo haya yote ndiyo yanayomfanya nabii Muhammadi kuwa shujaa au jagina wa dini ya Kiislamu sawia na Yesu katika dini ya Kikristo. Mfano wa miujiza hii ni pale ambapo tembe moja la mchanga lilitumika kuwaua watu kumi kwa pamoja (ub. 925-927).

Dini ya Kiislamu ina ushawishi mkubwa wa kumsilimisha kafiri na kumleta katika dini ya kweli.Wanajeshi wa Sufiyani waliamua kusilimu na kufuata dini ya kweli baada ya kuona vita vinaendelea kuwa vikali huku wakishindwa na wanajeshi waliotumwa na Mola kupitia nabii. Wanakiri imani ya Uislamu kwani wameona jinsi ilivyo na uwezo mkubwa vitani dhidi ya imani ya kuabudu miungu hivyo basi kukiri uwepo wa Mungu na mtume wake Muhammadi na kisha kuandamana nao Madina. Kinana na Kaaba nduguye walisilimu baada ya kung'amua ukweli wa imani yao. Kusilimishwa kwao kunaonyesha nguzo ya kwanza katika dini ya Kiislamu yaani shahada. Vilevile, nguvu za dini zinadhihirika wazi vita vilipofikia kilele chake. Wanajeshi wa Sufiyani walionusurika vifo walishurutishwa kukiri imani ya Uislamu na kuagizwa kupeleka jamii zao Madina, ili waweze pia kusilimu. Suala hili linadhihirisha kuwa dini inaweza kuwa na msukumo wa kubadilisha msimamo imara wa mtu pasi hiari kutokana na vitisho fulani kwa mfano kifo kama vile ilivyofanyika katika wahusika hawa wa upande wa Sufiyani ( ub.677,959 na 966).

Vita vya awamu ya kumi na moja vilidhihirisha nguzo ya kwanza ya dini ya Kiislamu ambayo ni shahada. Mikidadi anatumwa kwa nabii Muhammadi awaombee dua majeshi yake kwa Mola kwani vita dhidi ya makafiri vilielekea kuwashinda na kupitia maombi haya, ndiyo miujiza ya kuwashinda ilitendeka. Suala hili la dini linajitokeza wazi kupitia ushindi huo walioupata kutoka kwa nabii hasa kwa kutumia mchanga kuwatawanya makafiri hao (ub.916 na 932).

### 3.1.2 Ukafiri

Ukafiri ni kuasi na kuacha dini sahihi. Neno linalotumiwa sana katika dini ya Kiislamu likiwa na maana ya mtu asiyeamini na kushahidia kwa Mungu mmoja pekee na mtume wake Muhammadi. Ukafiri umejitokeza pale ambapo mhusika nguli Sufiyani anaabudu miungu pamoja na himaya yake yote.

Jamii ya Sufiyani imeishi katika kuongozwa na imani ya kuamini miungu ndio maana kulitokezea pingamizi kuhusu Abdirrahmani kujiunga na Sufiyani, kwani maovu waliotendea watu yalikuwa kinyume na imani ya Uislamu ambayo Abdirrahmani alikulia nayo alipokuwa kwao kabla ya kuasi Uislamu. Abdirrahmani alionyesha ukafiri alipoiasi dini ya kweli na kwenda kuabudu miungu kwa mfano 'lata'yaani miungu ambayo Maqureishi waliabudu kabla ya kukubali Uislamu (ub. 13).

Vita vya kidini vinaonyesha ukafiri kwani tofauti za imani ndizo zimesababisha vita.Kuamini miungu kunajidhihirisha wakati Abdirahmani na Sufiyani wanakuwa na tofauti hasa katika uamuzi alioufanya Abdirrahmani wa kumwachilia mwanawe Shamti alipozuiliwa. Tofauti hii ndio imepelekea Sufiyani na Abdirrahmani kukosana na ndio sababu Abdirrahmani akaamua kumuasi pamoja na dini yake ya kuamini miungu. Abdirrahmani ananena kuwa alikuwa amepotea katika imani ya dini na kwa hivyo anajihukumu moyoni kwa kuenda kinyume na sheria za Uislamu hasa ya kumfanya Muislamu mwenzake mtumwa (ub. 223-224).

Kushahidia dini yaKiislamu kunajitokeza kwa mara nyingine tena kwa wahusika kutoka upande wa Sufiyani. Kuuawa kwa Sufiyani na mwanajeshi wake Shemlani kulitokana na msimamo wao wa kidini kwani walikataa kukiri imani ya Uislamu na kwa hivyo kufa kwa kushikilia imani ya kuamini miungu ambayo ni ukafiri kulingana na dini ya Kiislamu. Sufiyani anasema hawezi kuisaliti dini waliyoiamini tangu jadi.

> Taturukuje sanamu
> Jadi yetu ya kadimu
> akanena muungamu
> Shekhe Ali kamwambia (ubeti 962)

### 3.1.3 Usaliti na Dhuluma

Usaliti ni kufanya jambo kinyume na matarajio ya makubaliano ilhali dhuluma ni hali ya kumnyima mtu haki anayoistahili kupewa au tendo la kufanyia mtu jambo lisilo la haki hivyo basi kumnyanyasa. Mdee *nw* (2011), wanaeleza dhana ya usaliti kama utoaji habari au ujumbe wa siri za nchi au mtu au hasidi wake. Wanaeleza zaida kuwa ni tendo la udanganyifu hasa unapomhadaa mpenzi wako kuwa unampenda ilhali ni uongo. Wameeleza pia dhuluma kama tendo la kumkataza mtu haki zake.

Usaliti na dhuluma umejitokeza katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwa njia mbalimbali, wahusika husika wakidhihirisha hulka zinazosawiri maudhui haya. Wahusika nguli ambao ni Abdirrahmani na Sufiyani wamedhihirisha usaliti na dhuluma kwa kiasi kikubwa katika utawala wao uliojaa maovu. Pindi tu Abdirrahman alipopewa mamlaka ya kusimamia wilaya, alitendea watu unyama kwa kuwaua wapita njia walipokosa kutii amri zake. Aliwanyang'anya mali zao njiani ndiposa akawa tisho kwa nchi zote. Vilevile, Abdirrahmani aliivamia misafara ya wafanyibiashara waliokuwa katika pitapita zao za kusaka riziki na aliyekataa kumpa alichokiitisha, alipigwa hadi kufa (ub.12 -21).

Makafikiri waliposhurutishwa kukiri imani ya Uislamu baada ya kushindwa vitani, ni thibitisho wazi kuwa walidhulumiwa kwani kila mtu ana haki ya kuamua masuala yake ya kiroho bila kulazimishwa. Makafiri hao walipigwa vibaya kutokana na uamuzi wao wa kiroho na hata wengine wao kuuawa kwa mfano Sufiyani.

Abdirrahmani amewasaliti wazazi wake kwa kupotea nyumbani bila idhini yao hivyo kuenda kinyume na sheria za babake na zaidi ya upotovu wake anakwenda nchi ya mbali ambayo anajihusisha na maovu jambo ambalo Abubakari babake alilikemea baada ya kupata malalamishi kuwa mwana wake anawateka nyara wapita njia na kuwanyang'anya miliki zao wanapotoka biashara zao na bila kusita aliamua kufunga safari kwenda kusuluhisha malalamishi hayo.

Mwana wa Abubakari
huyo tunayemdhukuri
lakini alihajiri
zamani akapotea (ubeti 11)

Usaliti wa kidini unajitokeza pale ambapo Abdirrahmani anakwenda kukiri imani ya kuamini katika miungu ilhali alikulia imani ya Uislamu inayoamini uwepo wa Mwenyezi Mungu ndiposa kutenda mabaya hakukumtisha kwa vyovyote vile kwani alikuwa ameiasi imani ya Uislamu (ubeti 13). Dini ya Kiislamu ni imani inayoshikilia kuwepo kwa Mungu mmoja pekee na hakuna mwingine anayestahili kuabudiwa ila yeye tu na mjumbe wake wa mwisho akiwa mtume Muhammadi hivyo basi kulingana na mafundisho ya Uislamu, Abdirrahmani alienda kinyume na sheria za dini hii.

Kama mwanao sadiki
kuwata ndia ya haki
akashika ufasiki
na wewe ukanyamaa(ubeti 82)

Kuzuiliwa kwa mtoto mdogo na Sufiyani pamoja na Abdirrahamani ni jambo baya linalokiuka haki za kibinadamu kwani kufungwa kwake kwa siku kumi na mbili kulikuwa adhabu ya babake baada ya kukosa kutimiza masharti yake Abdirrahmani bali sio ya mwana. Sufiyani aliagizia wachunga lango kumleta mvulana huyo ili auliwe. Alisimamishwa katikati ya watakaomuua huku mvulana huyo akipatwa na woga kuhusu ukatili atakaoupitia. Alilia akimwita babake Shamti kana kwamba anamwarifu kuwa maisha yake yalikuwa hatarini lakini mwishowe unyama huo haukufanyika kutokana na huruma iliomjia baada ya mvulana huyo kumtajia babake Abubakari kwa jina na uaminifu aliokuwa nao katika dini na zaidi ya hayo kuwa na uhusiano mzuri na nabii Muhammadi. Tendo la kumtishia maisha mwanawe Shamti ni kudhulumu haki zake na kwa hivyo ni kuenda kinyume na sheria za dini ya Kiislamu kama alivyofanya Abdirrahmani ( ub.177 -178).

Shamti bin Khadafu anatekwa nyara njiani na Abdirrahmani alipokuwa akienda kutafuta uelewa kuhusu mafundisho ya dini ya Kiislamu. Abdirrahmani alimwagizia dhahabu na vitu vingine na zaidi ya hayo alimzuilia mwanawe wa pekee hadi atakapopata vitu alivyoviitisha na pasi vitu hivyo angemuua. Huu ni unyama kwani kumnyima haki ya kuwa huru sio jambo linalostahili kutendewa binadamu yeyote. Shamti alipewa siku kumi kutimiza masharti ya mhuni huyu ya kuleta bidhaa hizo ndio maana mhusika huyu aliamua kutafuta usaidizi kutoka kwa nabii kwani hangeweza kutimiza alichotakiwa. Mafundisho ya Uislamu hayaruhusu mwislamu kumnyanyasa mwenzake. Vilevile, Shamti bin Khadafu anapatwa na mawazo mengi kuhusu jinsi atakavyomuauni mwanawe kutoka kizuizini.

Usaliti unajitokeza baina ya Sufiyani na Abdirrahmani pale ambapo Sufiyani anamuagizia Abdirrahmani kumuua mwanaye Shamti, kisha anamwachilia huru bila idhini yake Sufiyani jambo ambalo lilimghadhabisha na kumfanya kuapa kuwa iwapo angempata kokote alikoenda angemuua kwa kumkata shingo. Abdirrahmani hakunuia kumwachilia mvulana huyo bali ni huruma iliyomjia baada ya kutajiwa babake

Abubakari hili likiwa thibitisho kuwa anamheshimu kuliko bwana mkuu wake hata kuamua kusaliti amri yake.

Lau kama nampata
nti zote akapita
kitwa ningalimkata
hali ya kunitukiwa(ubeti 189)

Sufiyani anasaliti uhusiano wao mwema na Abdirrahmani kwa kumtusi babake Abdirrahmani, alipopata habari kuwa amri yake ya kumuua mvulana huyo haikutimizwa bali kaachiliwa baada ya Abdirrahmani kutajiwa babake- Abubakari kisha kuingiwa na huruma (ub.191-192). Vilevile, Abdirrahmani anamsaliti Sufiyani baada ya makubaliano yao ya kazi kutofanyika hasa ya kumuua mwanawe Shamti kama ilivyokuwa mazoea yao kufanya wanapowavamia wapita njia. Matokeo ya hasira ya Abdirrahmani yalimfanya kumsaliti Sufiyani bwana wake mkuu, pindi tu alipomtusi Abubakari babake kama chanzo cha kuachiliwa kwa mvulana huyo (ub.224).

Abdirrahmani anasaliti cheo chake alichopewa na Sufiyani kama mkuu wa wilaya. Sufiyani alimwamini sana kiasi cha kumpa mamlaka yake yote naye bila kusita alifanya kazi yake kwa uaminifu bila kutafakari kuwa kudhulumu watu lilikuwa jambo baya bali alifuata amri aliyopewa ndiposa baadaye aliamua kumuasi bwana mkuu wake. Bintiye Sufiyani anamkumbusha kuwa haikuwa sawa alivyokata kauli kwani baada ya kuaminiwa na kupewa usukani babake alistahili kupewa heshima wala sio usaliti kama huo.

Tunakupenda mapenzi
ukaitumia enzi
na hivi sasa huwezi
kwenu wataka rejea (ubeti 248)

Binti Sufiyani mkewe Abdirrahmani anamsaliti babake na kuamua kuandamana na mumewe kwenda Madina. Haya yalijiri pindi tu Abdirrahmani alipoamua kumuasi Sufiyani mkuu wake pamoja na dini yake ya uongo. Abdirrahmani alimuarifu mkewe nia yake ya kumwacha babake na enzi zake zote na kumrai aandamane naye jambo ambalo mkewe hakulikataa na zaidi ya kukubali kumwacha babake, aliamua kusilimu

na kukiri imani ya Uislamu kabla ya kufunga safari. Kumsaliti babake pamoja na dini yake kulizua vita kama njia ya kumkataza kwenda na mumewe.

Tashahadia Mungu
nimtupe baba yangu
nenende na mume wangu
kwa Muhammadi rasua(ubeti 251)

Abdirrahmani anausaliti uhusiano wa kijamii unaotokana na kuozwa kwake kwa binti Sufiyani. Kutokana na mila za jamii mtu huheshimu alikooa na kudumisha uhusiano huo daima yaani mtu na mkwewe huwa na mbeleko ya hali ya juu lakini matendo ya Abdirrahmani baada ya kukosana yalipita mipaka hata kumchukua binti Sufiyani bila idhini yake na pia licha ya hayo, kabla ya kuanza safari yake ya kwenda Madina alitangazia majirani hadharani kuwa anaondoka na kuwa Sufiyani apewe ujumbe huo na pia aambiwe wazi kuwa amemchukua bintiye. Hali hii sio ya kutarajia hasa kwa mtu na mkwewe kabla ya kuwa na tofauti zinazowatenganisha kwani wote walifaa kuwa jamaa moja. Katika ndoa za jamii nyingi, jamii yote huhusishwa pamoja na wakuu wao ili kufanikisha shughuli hiyo, kwa hivyo Abdirrahmani aliisaliti jamii yote kwa jumla kama wahusika wakuu walioshughulika alipokuwa akifunga ndoa (ub. 277-297).

Abdirrahmani anadhulumiwa na Sufiyani kwa kunyimwa haki ya kuteua kile roho yake imeamua. Kuiasi dini inayoamini miungu ilikuwa hiari yake kwani masuala ya kiroho binadamu halazimishwi. Anapigwa vita hata mwishowe kuumia vibaya alipokuwa katika safari yake ya kwenda kuridhiana na wazazi wake pamoja na dini ya kweli. Binti Sufiyani kukubali kuandamana na mumewe Abdirrahmani ulikuwa pia uteuzi wa moyo wake hivyo basi hakukuwa na lazima ya babake kumfuata na kuzua vita dhidi ya Abdirrahmani.

Wakafika jabalini
Jeraha za muilini
zimemshika yakini
hawezi kujondolea (ubeti 452)

Mhusika Kinana na nduguye Kaabu wanamsaliti Sufiyani kwa kukubali kuungana na Mikidadi na jeshi la nabii. Huu ni usaliti kwani Sufiyani ndiye alikuwa amewatuma

kama jeshi lake hodari kupigana vita dhidi ya majeshi ya nabii lakini badala yake wanakubali kushawishiwa na Mikidadi. Mikidadi alijulikana kwa ushujaa wake vitani sawia na Kinana na nduguye hivyo, basi Sufiyani akawa na matumaini makubwa kuwa wangeshinda vita jambo ambalo likawa kinaya kwake baada ya wanajeshi wake hawa wawili kukubali kuungana na hasimu wake. Wanajeshi hawa waliamua kufanya usaliti huu kwa kuhofia kuuawa vitani kwa hivyo kumsaliti bwana mkuu wao Sufiyani ikawa suluhu ili kukwepa.

Tufanyeje ndugu yangu
twepukane na matungu
shauri lako ni langu
nduguye akamwambia (ubeti 668)

Vilevile Kinana na nduguye wanaisaliti dini yao yaani dini inayoamini miungu na kukubali kukiri imani ya Uislamu. Wanapoona kuwa nguvu za majeshi ya nabii zinawazidi wanaamusa kuungana nao na kukiri imani hiyo, kichocheo kikubwa kikiwa woga wa kupigwa na wanajeshi wa upande wa Abdirrahmani kitendo ambacho kingeleta majeraha au kufa. Hali ya vita inawawia ngumu kiasi cha kubadili imani yao baada ya kupatwa na hofu moyoni itokanayo na vitisho walivyovipata (ub. 677 na 681).

### 3.1.4 Ndoa na Mapenzi

Ndoa ni muungano wa mume na mke katika kuanzisha aila yao. Asasi ya ndoa ndiyo huendeleza vizazi katika jamii hivyo basi jamii huongezeka na kupanuka kupitia asasi ya aina hii. Kulingana na masuala ya dini ya Kiislamu, ndoa ni mapatano ya kisheria kati ya mwanamume na mwanamke na ambayo hufanywa kwa njia ya mkataba wa ndoa. Wakati mwingine, mapatano haya huwa kwa njia ya maandishi na yanashuhudiwa na mashahidi wawili na mlezi wa bibi arusi. Vilevile dini ya Kiislamu hutilia moyo suala la ndoa kwa kukumbuka tamko la mtume Muhammadi aliposema kwa vijana kuwa, aliye na uwezo wa kuoa aoe kwani kufanya hivyo kungesaidia kuepukana na uasherati.. Aya mbalimbali za Qur'an zinaeleza kuwa Mungu ameumba waume kwa wake ili pamoja kwa mapenzi, wazae watoto na waishi kwa amani na utulivu.

Maudhui ya ndoa na mapenzi katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* yamejitokeza pale ambapo mhusika Abubakari na mkewe walivyomlea Abdirrahmani kwa njia ya dini na uadilifu. Abdirrahmani kuwa na dada anayeitwa Ayesha wa toka ni toke ni thibitisho wazi kuwa Abubakari anaishi katika maisha ya ndoa iliyo imara inayoongozwa na imani ya Uislamu. Kutoroka kwa Abdirrahmani akiwa na umri mdogo hakukumfurahisha babake kwani alikuwa bado anahitaji malezi bora kutoka kwa wazazi wake (ub. 10).

Suala la ndoa linajitokeza kati ya Abdirrahmani na binti Sufiyani. Baada ya Abdirrahmani kuishi na Sufiyani kule alikokuwa ametorokea, alipewa uongozi na hatimaye kuozwa bintiye Sufiyani. Kuozwa kwake kwa bintiye Sufiyani ambaye ni mwana wa mkuu wake aliyempa utawala huu, kutokana na uaminifu wake kazini kwani aliyafanya yote aliyotaka mkuu wake pamoja na kuabudu miungu kama vile himaya hiyo ilivyofanya. Ndoa yao ilijengeka katika misingi ya mapenzi ya dhati jambo ambalo liliwaweka pamoja katika wakati wa raha na shida. Hali hii ni dhahiri kwani licha ya Sufiyani kumwoza bintiye, ni lazima pia mwenyewe alimpenda na kukubali posa yake ;kwani masuala ya ndoa hutegemea mapenzi ili kudumu licha ya kulazimishwa.

Kaoa mwana nyumbani
mtoto wa Sultan
bintiwe Sufiyani
ndiye aliyemuoa (ubeti 14)

Ndoa baina ya Abubakari na mkewe inaonekana kujengwa katika misingi ya dini hili likiwa dhihirisho kuwa uadilifu uko katika familia yake. Suala la dini ndilo huleta mafanikio katika malezi bora katika ndoa. Uhusiano mwema kati ya Abubakari na mkewe umeonekana pale ambapo mkewe anamwombea mumewe kwa Mola asafiri salama alipokuwa akienda kumwokoa mwana wao Abdirrahmani kutoka maovu yaliyokuwa yamekithiri hata kutatiza amani ya nchi. Mapenzi ya dhati yanadhihirika katika ndoa hii hivyo kuleta amani baina yao (ub. 93 - 97).

Na mkewe akaombea
Muumbuwa akiumba
takunusuru na simba
na makaa yote pia (ubeti 96)

Binti Sufiyani aliamua kuandamana na mumewe kwenda Madina baada Abdirrahmani kukosana na babake. Ndoa yake na Abdirrahmani inadhihirika wazi kuwa ilikuwa ya mapenzi ya dhati kwani kumsaliti babake mzazi pamoja na amri yake ya kumkataza kwenda na mumewe hakukufua dafu na kwa hivyo akafunga safari na kuelekea Madina. Pia kuacha imani yake na kusilimu ni ishara tosha kuwa ndoa hii ilijengeka kwenye msingi imara wa mapenzi. Binti Sufiyani anasema kuwa hawezi kumwacha mumewe kisha abaki katika hali ya upweke, ndio maana alijiandaa vyema kwa minajili ya safari (ub. 250, 258, na 259).

Uhusiano mwema katika ndoa unaonekana vitani pale ambapo Abdirrahmani anajeruhiwa kisha mkewe binti Sufiyani anaanguka kwa kuhuzunika na kupandwa na hasira. Akajitayarisha kwenda kupigana na jeshi la babake na hatimaye kuwaua idadi yao kubwa sana. Mapenzi baina yake na mumewe yanadhihirika hasa kutokana na hisia zake baada ya mumewe kuumia. Moyo wake ulijaa kihoro alipoona majeraha ya Abdirrahmani yamemletea maumivu makali hata kumfanya kutoenda vitani.

Angalia makafiri
na mume wangu mzuri
amekwisha mkhasiri
sefu yangu niletea (ubeti 439)

### 3.1.5 Ushujaa / Ubabe

Ushujaa ni hali ya kuwa na ujasiri wa kufanya jambo bila woga kwa hivyo shujaa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo hata kama ni hatari yaani ni mtu jasiri, nguli, jogoo, jabali na n.k.

Mdee *nw* (2011), wanasema ushujaa ni hali ya kuwa na moyo wa ujasiri. Tunaafikiana na maelezo haya kwa kusema kuwa ushujaa ni hali ya kuwa na moyo wa kutenda mambo pasi woga yaani kuwa na uhodari na ukakamavu katika utendaji wa mambo. Ushujaa / ubabe umejitokeza katika mhusika nguli Abdirrahmani aliyepotea akiwa na umri mdogo na kwenda kuishi na Sufiyani kiongozi kafiri. Kutoroka kwake hakukuwa jambo la kawaida kwa mtoto aliyelelewa katika maisha ya dini hasa kuamini Mungu. Pia kwenda safari ya mbali bila idhini ya wazazi wake ilikuwa ishara ya ushujaa au ujasiri.

Alipotea zamani
akenda kwa Sufiyani
kwa babaye akahuni
ali kijana sabia (ubeti 12)

Ujasiri unadhihirika pale ambapo Abdirrahmani anakuwa kiongozi katika himaya ya Sufiyani, kwani alijulikana kutokana na ujasiri wake na unyama aliowatendea wapita njia. Hakuna aliyethubutu kumkosea kwa njia yoyote ile kwani alikuwa katili ajabu hadi ya kuwa akikosewa hangesita kutoa adhabu ya kifo. Alivamia misafara ya wafanyabiashara njiani na kuwanyang'anya mali yao yote bila kujali matokeo yake. Alikuwa tisho kwa nchi nzima hata kukimbiwa na Warumi na Wamisri wamwonapo njiani.

Kawa shujaa mkali
wala asiye wa pili
asizumbuke rijali
mwenye kumtaadia (ubeti 16)

Akavunda misafara
katika ndia za bara
akawapoka tijara
zote akazitukua (ubeti 19)

Kutekwa nyara kwa mwanawe Shamti na kisha kuachiliwa na Abdirrahmani kinyume na amri ya bwana wake mkuu Sufiyani ilidhihirisha ujasiri na ukakamavu wa Abdirrahmani kwani hakuna mtu yeyote angeweza kupingana na Sufiyani kutokana na ukatili wake dhidi ya watu. Sufiyani alijulikana nchi zote hasa kwa kudhulumu watu pasi mbasi lakini Abdirrahmani hakuogopa uamuzi alioufanya.

Muateni ende zake
na tena msimshike
kijana kutoka kwake
kwa mbio akakimbia (ubeti 181)

Wanajeshi wa Sufiyani wanaonyesha ubabe wao walipoagiziwa na mkuu wao kumfuata bintiye Sufiyani baada ya kutoroshwa na Abdirrahmani. Sufiyani anakusanya majeshi yake elfu ishirini na kuwaagiza wajitayarishe kwa silaha kali kwenda kumsaka bintiye kisha wote wansatii amri na kuanza safari yao. Ujasiri huo wao ndio uliowafanya kufanya upesi kwenda kukabiliana na adui msituni. Majeshi hawa walijiandaa kwa kubeba mikuki yao kila mmoja akitetema kutokana na hisia za hasira.

Wakangiya shujaani
bi tarifati aini
jumlaye ishirini
alufu zikatimie (ubeti 286)

Safari ya kuondoka kwa Abdirrahmani na mkewe ilionyesha ushujaa kwani matayarisho yao yalikuwa ya hali ya juu. Wote walijifunga libasi na kuweka ngao tayari kwa safari na pia kukabiliana na adui yeyote njiani Sufiyani akiwemo. Tunaelezewa pia kuwa mkewe Abdirrahmani alikuwa na ubabe wa kipekee kutokana na matayarisho hayo ya safari kwani wote watatu walijifunga vilivyo kwa kuweka tayari ngao zao na panga. Ujasiri huu ulionekana wazi kutoka kwa wahusika hawa watu: Abdirrahmani, mkewe binti Sufiyani na Mora rafikiye Abdirrahmani. Pia kusafiri usiku kucha kunaonyesha ubabe wao hasa katika kukabiliana na jambo lolote ambalo lingeweza kutokea njiani. Safari hii ni ya ushujaa kwani shujaa hatishiki na lolote litakalotokea njiani. Wahusika hawa walipanda na kushuka milima na mabonde usiku wote bila kukata tamaa. Mora aliwaongoza katika safari hiyo, hivyo basi anadhihirisha ushujaa.

Ushujaiwe harume
ni sawasawa na mume
nyamaza usiseme
sifaze hikusifia (ubeti 261)

Ujasiri wa Abdirrahmani unajitokeza pale ambapo anakabiliana na Sufiyani akimsihi arudi baada ya tofauti zao kupita mipaka kisha anamjibu bwana mkuu wake kwa ukakamavu kwa kusema amwondokee na upumbavu na udhalimu wake kwani hana haja nao kabisa. Hili ni dhihirisho wazi kuwa hamwogopi Sufiyani kwa vyovyote vile licha ya cheo, ukwasi na hata unyama alionao unaomfanya kuogopwa na nchi zote na pia kumtusi mkwe kunahitaji mtu mwenye ujasiri kama alivyofanya.

Kamjibu kwa ukavu
kwa maneno ya nguvu
Sufiyani mpumbavu
hayo usingenambia (ubeti 342)

Ushujaa wa Abdirrahmani unajitokeza sana hasa katika vita alivyopigana baada ya kukaidi amri ya Sufiyani ya kumrudia na pia kilichozidisha zaidi ufidhuli wa Sufiyani ni bintiye kukataa kurejea kwake akidai kuwa lazima aandamane na mumewe kwenda

Madina kwenye dini ya kweli. Abdirahmani kumvamia Sufiyani katika jaribio la vita vya awamu ya kwanza kulidhihirisha ubabe wake kwani tumeelezewa kuwa alimvamia kama simba jambo ambalo mtu wa kawaida hangethubutu kufanya.

Na Abdirrahmani
kamwendea Sufiyani
kama simba ghadhbani
Sufiyani kakimbia (ubeti 361)

Jaribio la pili la vita lilikuwa baina ya wanajeshi wa Sufiyani na Abdirrahmani lakini aliwavamia vivyo hivyo hadi wakatorokea mafichoni licha ya idadi yao kubwa ndio sababu Sufiyani akakasirika na kusema kuwa itakuwa aibu kwao kwenda kusema walishindwa vitani na nguvu za mtu mmoja tu yaani Abdirrahmani hivyo basi ubabe wake unadhihirika wazi.

Sufiyani akanena
Jeshi mliokutana
mwafukuzwa na kijana
huyule mtu mmoya (ubeti 366)

Abdirrahmani anaingia vitani katika awamu ya nne na kutokana na ukakamavu wake, aliwaua majeshi wa Sufiyani elfu kumi dhidi ya kuongezeka kwa idadi yao. Tumeelezewa katika utenzi huu kuwa vita hivyo vilianza alfajiri hadi jioni bila kupumzika. Kutokana na ubabe wake, tumepata pia taswira ya mambo halisi hasa alipowakata vichwa adui zake na kisha wakaanguka kama mvua. Kituko hiki kiliwashangaza walionusurika kifo kwani waliweza kutambua ushujaa wa Abdirrahmani (ub.421-423).

Mora anathibitisha ushujaa wa Abdirrahmani kutokana na yale maneno aliyoyanena kule milimani baada ya Abdirrahmani kurejea kutoka vitani. Mora anasema kuwa anashangazwa na nguvu alizonazo Abdirrahmani hata kuwafurusha wanajeshi wa Sufiyani. Anaeleza kuwa hajawahi kuona mtu yeyote akienda vitani akiwa na ujuzi na ujasiri kama wake. Vilevile, Mora anaendelea kunena kuhusu ushujaa wa Abdirrahmani kwa kusema kuwa, ana upekee ambao hajawahi kuuona kwingine aendapo vita hivyo basi hakuna anayeweza kufananishwa naye (ub. 397-399).

Binti Sufiyani anaonyesha ujasiri wake pale alipoenda kupigana na majeshi ya Sufiyani hata kuwaua watu elfu msbili mia tano kwa sekunde mbili. Ushujaa wake vitani ulipelekea wanajeshi wengine kuzimia na wengine kufa kutokana na hasira zake. Mwanamke kwenda vitani pekee na kushinda wanaume wenye ujuzi halikuwa jambo la kawaida hivyo kumfanya shujaa. Ujasiri wake vitani uliwafanya watu kuulizana kuhusu binti Sufiyani hasa alikotoka kwani hawakuamini jinsi mtu mmoja anavyoweza kuupiga umati mkubwa na zaidi ya hayo, ni kiumbe hafifu mbele ya mwanamume.

Muda wa dakikateni
kaua Shujaani
jumlaye alfeni
kuzidi khamsumia (ubeti 448)

Watu wakaulizana
nani mwenye kuuwana
aliye shujai sana
azidiye watu pia? (ubeti 449)

Mikidadi anaonyesha ushujaa wake vitani kwa kuwaua wanajeshi wa Sufiyani elfu sita kwa muda mfupi. Ushujaa wake ndio ulimfanya atumwe na nabii kumuauni Abdirrahmani aliyekuwa amepata majeraha mabaya. Ujasiri wake uliogopwa na shujaa anayetambulika kote miongoni mwa wanajeshi wa Sufiyani hivyo basi kushangazwa na uvamizi huo wa Mikidadi na kuamua kusilimu na kukiri imani ya Uislamu. Kisa hiki kimebainisha wazi kuwa, Mikidadi aliingia uwanja wa vita kama mvua na radi na kuzua vita vikali vya kuogofya. Anawaeleza kuwa hawatadhurika kwa njia yoyote ile bali watakuwa jamii moja katika Uislamu. Ushujaa wa Mikidadi ndio uliwatishia kubadili dini (ub.637 -673).

Vilevile ushujaa unaonekana katika mhusika Shemlani mwanajeshi hodari wa Sufiyani kwani walipopigwa na jeshi la nabii, Sufiyani anatumana aje ili akabiliane vikali na upande wa Abdirrahmani. Shemlani aliweza kujigamba mbele ya jeshi lililotumwa na nabii bila kujali lolote hivyo kuonyesha ubabe wake waziwazi na pia Warumi na Wamisri walimjua tangu jadi kutokana na ushujaa wake vitani. Mashujaa hawa walitambulika katika jamii walikotoka lakini baada ya vita hivyo, ushujaa wa Abdirrahmani ulionekana kuliko wa Shamlani kwani alimshinda.

Kutokana na maelezo ya hapo awali kuhusu sifa za shujaa, tunapata kuoanisha safari ambayo wanajeshi wa nabii walifunga kuelekea vitani ili kumuauni Abdirrahmani kama ushujaa. Mikidadi, Abbasi, Fadhili na wenzake ni mashujaa wa vita waliotumwa na nabii kwenda nyikani alikokuwa Abdirrahmani safari iliyowachukua muda mrefu. Wahusika hawa hawakujali lolote njiani kwani walikuwa askari wenye ujuzi wa kukabiliana na adui yeyote bila woga hivyo basi kudhihirisha wazi safari ya mashujaa au majagina wa vita.

Safari ya mashujaa huhitaji matayarisho ya kutosha kwani huchukua muda mrefu kabla ya kukamilika. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umeonyesha safari mbalimbali za mashujaa katika harakati zao za vita na miongoni mwao ni kama vile Abdirrahmani, Mikidadi, Fadhili na wengine. Mashujaa hawa wote walijipamba kwa mavazi yao ya vita kisha wakapanda farasi tayari kwa lolote njiani. Vita vilikuwa mizani ya kupima ushujaa wa mhusika fulani hapo jadi ndio maana kila jamii ilikuwa na shujaa wao (ub.523 na 631).

Abubakari anaonyesha pia ushujaa anapopanga safari ya kwenda kumsaka mwanawe katika nchi nyingine na kuwa na matumaini ya kufika alikokuwa licha ya kujua kuwa ni safari itakayomchukua siku nyingi. Huu ni ujasiri wa mashujaa kwani mashujaa huhusishwa na safari hasa ya kusaka jambo au kitu fulani bila kukata tamaa.

Na mkewe akaomba
muumbuwa akiumba
takunusuru na simba
na mabaa yote pia (ubeti 96)

Shamti bin Khadafu anaonyesha safari ya mashujaa kwa kupanga mipango yake vyema na kisha kuaga jamii yake kwa minajili ya safari ndefu aliyokuwa nayo ya kwenda Madina. Nia ya safari yake ilikuwa kusaka utulivu wa moyo wake kupitia dini lakini kabla ya kuafikia lengo lake, anakumbwa na matatizo njiani ya kutekwa nyara na Abdirrahmani. Safari hii ni ya ushujaa kwani sifa kuu ya mashujaa ni kukumbwa na changamoto njiani ambazo wanajinasua hatimaye kama ilivyomfanyikia mwarabu huyu na mwanawe. Shamti ni shujaa wa kidini kutokana na safari yake na imani yake ya kuamini kuwa mwanawe ataachiliwa.

Mfano mwafaka kutoka utenzi huu ni pale ambapo Shamti anaeleza jinsi alivyofunga safari na mwanawe ili apate kujua zaidi kuhusu dini ya kiislamu ingawaje alipata kizuizi njiani yaani Abdirrahmani (ub.54-56).

Safari ya Abdirrahmani na mkewe binti Sufiyani ina sifa ya ushujaa kwa sababu wanasafiri mchana na usiku kuelekea Madina na baadaye kukumbwa na matatizo ya kuvamiwa na majeshi ya Sufiyani baada ya kuiasi dini ya bwana mkuu wake na kisha kuondoka bila idhini yake. Safari hii ilikuwa ya watu watatu Abdirrahmani, binti Sufiyani na Mora na wote wakawa wana ujasiri wa kusafiri katika njia iliyojaa wanyama wa mwitu bila woga. Thibitisho la kuonyesha kuwa safari hii ilikuwa ndefu, ni pale walipopumzika kwenye jabali baada ya kupanda na kushuka milima na mabonde bila kupoteza matumaini ya kwenda Madina (ub.264-267).

Sufiyani anaonyesha ushujaa wake anapoamua kufunga safari ya kwenda kumsaka bintiye aliyekuwa ametoroka na Abdirrahmani bila ruhusa yake. Safari yenyewe ilikuwa ndefu tena yenye milima na mabonde iliyojaa misitu lakini aliipitia vivyo hivyo akiwa na lengo moja la kumregesha mwanawe. Ukakamavu na ujasiri wake ndio unamfanya kuwa shujaa kwani alikuwa tayari kufanya lolote lile mradi ampate mwanawe.

> Akapanda farasi
> kamba twendeni upesi
> tumwandamie mtesi
> mwanangu alomtwaa (ubeti 290)

Nabii Muhammadi ni shujaa mkubwa wa dini katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwani ndiye mwenye kupokea uwezo kutoka kwa Mungu na kuweza kufanya miujiza kwa binadamu. Kuponywa kwa Abdirrahmani kwa majeraha aliyoyapata vitani, pamoja na Abbasi kuwaua makafiri kwa kutumia mchanga kunaonyesha ushujaa wa kidini. Hii ni miujiza ambayo binadamu wa kawaida hawezi kufanya. Vilevile majeshi wote waliotumwa vitani na nabii walipigana kwa njia isiyo ya kawaida na kuwaua wapinzani wao wengi kwa dakika chache hivyo basi hii ni ithibati tosha kuwa nguvu hizi ni za kimiujiza.

Akenda akamshika
alimo kudhurubika
jeraha zikiondoka
mara moja akapoa (ubeti 622)

Tembe moja ya mtanga
ashikayo mwenyi anga
hawachinyangachinyanga
na farasi wote pia (ubeti 927)

### 3.1.6 Vita

Vita ni hali ya kupigana kwa silaha au maneno baina ya pande mbili au zaidi zinazokinzana kimawazo. Vita huletwa na tofauti za wanajamii katika harakati zao za kukidhi mahitaji yao ya kila siku hivyo basi tofauti hizi zinaweza kuwa za kiuchumi au kisiasa au hata masuala ya kijamii kama vile dini ilivyo katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Tofauti za kidini ndizo zimeleta mkinzano mkubwa miongoni mwa wahusika. Wahusika hupitia changamoto mbalimbali katika maisha ambazo huwapa msukumo wa aina fulani wa kusaka uhuru wao au haki zao ili kuleta mabadiliko na mafanikio ya maisha kwa jamii iliopo na hata jamii ijayo hivyo basi mageuzi haya hayatokei pasipo na vita kwani mvurugano na mvutano ndio huleta ushindi.

Vita vya maneno na silaha vilijitokeza mno kwenye *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* pale ambapo tofauti zinazuka baina ya Sufiyani na Abdirrahmani kuhusu kuachiliwa kwa mwanawe Shamti jambo ambalo lilipelekea babake Abdirrahmani kutusiwa hivyo kumlazimu Abdirrahmani kutofautiana na bwana mkuu wake. Vilevile mawazo yao yalitofautiana ndiyo yalizua vita vya silaha, vita vya maneno vikichochea zaidi. Sufiyani anaonyesha dharau na kiburi kwa Abdirrahmani licha ya kumfanyia kazi vizuri. Abdirrahmani alimtii bwana mkuu wake hadi wakati alipoamua kutoka kwake na kurudi kwao Madina. Uamuzi huo haukuwa jambo la Sufiyani kunena maneno makali juu yake pamoja na kumtusi babake Abdirrahmani. Maneno haya yote yanadhihirisha vita vya maneno kama chanzo cha vita vya silaha (ub. 191-192).

Ushindani baina ya Abdirrahmani na Shamti bin Khadafu kuhusu dhuluma waliotendewa na Abdirrahmani unazua vita vya maneno hasa wanapojibizana kuhusu kuzuiliwa kwa mwanawe Shamti na hata kutishiwa kuuawa pasi kutimiza masharti ya

Abdirrahmani. Shamti anamsihi amwachilie na asimdhuru kwani alikuwa radhi kumpa chochote alichokuwa nacho mradi aachiliwe akiwa salama lakini alijibiwa kwa ukali kuwa aende zake lakini mwanawe atazuiliwa. Hali hii inaonyesha kuwa kuna vita vya maneno baina yao na zaidi ya hayo mawazo yao yalikuwa yanapingana kutokana na tofauti hizo.

Kanijibu kwa ukali
enenda zako ajali
wa ama yako ayali
sitaweza kukwatia (ubeti 57)

Maandalizi ya Abdirrahmani ya kuondoka kwa Sufiyani yalionyesha wazi kuwa alikuwa tayari kwa vita vitavyotokea kutoka kwa bwana mkuu wake hasa baada ya kumwasi. Vilevile, bintiye Sufiyani kumsaliti babaye na kuandamana na Abdirrahmani ilikuwa sababu tosha ya kumtayarisha dhidi ya vita vitakavyozuka baina yake na wanajeshi wa Sufiyani hivyo basi akajifunga silaha zote zitakazomsaidia njiani katika safari yake ya kurudi Madina.

Tumeelezewa kutoka kwenye utenzi kuwa Abdirrahmani alijivika libasi na kisha yeye na wenzake wakajifunga ngao zao na upanga. Matayarisho haya yote yalionyesha vita vya silaha kwani ilikuwa wazi kwamba Sufiyani hangemruhusu bintiye kwenda na adui yake. Ngao na upanga ni ishara ya kuwa na vita kati ya wahusika hawa kwa hivyo matayarisho yao yalilenga kufaulu vitani ( ub. 260-262).

Abdirrahmani anaenda kukabiliana na Sufiyani na jeshi lake milimani walikokuwa wamepumzika kabla ya kuendelea na safari yao ya Madina. Anakabiliana na Sufiyani kwa maneno akitaraji kupigana naye kwani alikuwa tayari kwa lolote hata kumuarifu Mora kuwa afapo kwenye vita, amfikishe mkewe Madina ingawaje nia yake haikuwa kuzua vita ndiposa kabla ya kwenda anamsihi Mola wake mwenye uwezo juu ya binadamu asimwingize vitani. Kifo kwa kawaida ni tokeo la vita panapokuwa na ushindani wa aina fulani ndio maana Abdirrahmani anatayarisha nafsi yake kwa kumwambia rafiki yake kuwa anapokufa, amfikishe mkewe Madina kwa wazazi wake. Vilevile, Abdirrahmani anonyesha kuwa kuna vita anapomwambia Mora kuwa asijiingize vitani (ub. 298 -299).

Kuna vita vya maneno baina ya Sufiyani na bintiye kwani anaambiwa na babake kuwa asiandamane na Abdirrahmani mumewe kule kwao Madina. Wanajibizana kwa muda mrefu huku akishikilia kuwa harudi na isitoshe amesilimu hivyo basi ameiasi dini ya babake ya kuamini miungu. Bintiye anampiga vita babake kwa maneno kwa kumwambia kuwa alipomuoa mamake alimchukua na kwenda naye kwake wala hakurejea kwao baadaye jambo ambalo lilimshinda babake kujitetea. Bintiye Sufiyani anajaribu kutoa sababu ambazo zinamfanya asibaki na babake bali aende na mumewe Madina. Binti Sufiyani anamjibu babake kuwa, alipomuoa mamake alimfuata na kuishi naye kwake bali hakuishi na wazazi wake kwa hivyo hana budi kumruhusu aandamane na mumewe.

Yule kijana kasema
ulipomuoa mama
naye kwao alihama
akaja kukufwatia (ubeti 355)

Vita vya silaha baina ya Abdirrahmani na Sufiyani vilianza pindi Sufiyani alipogundua kuwa mwanawe akaidi amri ya kwenda naye nyumbani. Maudhui ya vita yamejikita sana katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Abdirrahmani alimvamia Sufiyani kama simba kisha Sufiyani akaamua kutoroka kwani aliona vita vinamshinda. Hivi ndivyo vilikuwa vita vya kwanza kuzuka. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa vita katika awamu ya kwanza kwani vita vilijitokeza katika awamu mbalimbali (ub.361-362).

Vita katika awamu ya pili vilihusisha jeshi la Sufiyani na Abdirrahmani ambapo anawashinda jambo ambalo lilimfanya Sufiyani kuwakemea akidai kuwa ni aibu mtu mmoja kuwapiga kwani aliamini walikuwa na ujuzi wa kutosha. Sufiyani anawazomea wanajeshi wake akidai kuwa hawana uchungu wa mwana hivyo basi akaamua kwenda vitani pekee alipoona wanajeshi wake hawakujikaza vitani. Sufiyani ananena kuwa haiwezekani kijana mmoja kufukuza jeshi zima ambalo limekutanisha mashujaa wake. Anapandwa na hasira inayotokana na uchungu wa kumpoteza mwana, na hivyo anaamua kuwa na ukakamavu wa kuonana uso kwa uso na shujaa Abdirrahmani kama alivyosema kuwa atampiga vibaya sana ( ub. 366-369).

Katika awamu ya tatu ya vita, Sufiyani anajitokeza na hata kabla ya kukabiliana na Abdirrahmani analia na kumtusi kwa kumchukua mwanawe. Anamwambia kuwa hana shukurani licha ya kumstarehesha nyumbani kwake kwa kumpa cheo kikuu na wasaidizi wengi. Anamwambia kuwa uzoevu wa kuishi kwa umaskini ndio umemfanya kutotosheka na anachopewa na hivyo anajuta kumwoza bintiye.

Mzoele ufakiri
kazi yenu kwenda shari
hamwezi utajiri
hata mjapoupewa (ubeti 374)

Sufiyani anaanguka miguuni mwake Abdirrahmani wakati wa vita hivyo kisha jeshi lake linakuja kumsaidia lakini Abdirrahmani anawakatakata hata wengi wao kufa. Mauaji hayo yanaendeleza vita zaidi kwani Abdirrahmani alifahamu wazi kwamba majeshi ya Sufiyani hayamwezi licha ya kuongeza idadi yao. Majeshi ya Sufiyani yalikuwa na wanaume wenye ujasiri, ujuzi na uzoefu katika vita lakini Abdirrahmani aliwaua wengi na wakafa kama mbwa. Vita hivi viliendelea kutoka mchana hadi jioni na kusababisha vifo elfu sita. Muda ambao vita vilichukua ulidhihirisha uadui ambao wahusika hawa walikuwa nao ndiposa vifo vingi vilishuhudiwa kati yao.

Kulipofunga dhulamu
waliokenda kuzimu
sita elfu fahamu
watu aliowaua (ubeti 394)

Baada ya wanajeshi wa Sufiyani kushindwa katika vita vya awamu ya tatu, majeshi elfu kumi waliongezeka lakini kutokana na ubabe wa Abdirrahmani, aliwaua watu elfu kumi kwani vita hivyo vilianza alfajiri hadi jioni bila mapumziko na hivi ndivyo vilikuwa vita katika awamu ya nne. Mfano mwafaka wa kuonyesha kuwa kulikuwa na vita ni pale ambapo tumeelezewa kwamba, Abdirrahmani aliwakata adui zake vichwa wakaanguka kama mvua ndio maana wakatambua ushujaa wake vitani ( ub. 421-423).

Mhusika Amiri mwanajeshi hodari wa Sufiyani aliingia vitani katika awamu ya tano ili kupimana nguvu na Abdirrahmani. Walikuwa wamepigana bila kupumzika kuanzia asubuhi hadi adhuhuri ndiposa Amiri akatumwa kuwasaidia wanajeshi waliokuwa

wakiendelea na vita dhidi ya Abdirrahmani lakini walishindwa vivyo hivyo. Walijeruhiwa na wengi wao kuuawa.

Kamtokea kafiri
jina aitwa Amiri
ni shujai mashhuri
katika bani rumiya (ubeti 428)

Kuongezeka kwa idadi ya wanajeshi wa Sufiyani kulionyesha vita katika awamu yake ya sita na ilipofika asubuhi wanajeshi hawa walikuwa wamewasili wakiwa wamejiandaa kumuauni Sufiyani vitani. Nguvu za majeshi ya Sufiyani yakamzidi Abdirrahmani na kupata majeraha hivyo basi kukosa nguvu za kuendelea vitani na kupelekea kushindwa kwake ( ub. 432-433).

Binti Sufiyani amekuwa mhusika mkuu katika vita vya awamu ya saba ambapo anashika usukani baada ya Abdirrahmani kujeruhiwa. Anamkata mmoja wa askari wa Sufiyani hadi kumtoa kichwa na kisha akawaendea wanajeshi wengine ambao walishtuka hadi kuzimia kutokana na hasira zake. Wanajeshi hawa walishangazwa na mwanamke huyu kwani kwa muda wa sekunde mbili, alikuwa ameua wanajeshi elfu mbili mia tano. Mauaji haya vitani yalileta vitisho kwa wahusika walionusurika kifo.

Vita katika awamu ya nane viliendelea binti Sufiyani akipambana na wanajeshi wa Sufiyani kwa mara nyingine na ambapo anawajeruhi wengi na elfu mbili wakiuawa. Sufiyani anapoona bintiye ndiye mhusika mkuu katika vita hivi anawasihi wanajeshi wake wasimuue bali wamshike lakini yote yaliambulia patupu kwani aliwaua elfu moja zaidi. Usaliti wake binti Sufiyani ulikuwa umekithiri hata kiasi cha kutomjali babake mzazi ambaye alidhani kuwa hangemdhuru lakini yote yakawa kinyume na matarajio yake. Sufiyani anathibitisha jinsi vita vilikuwa vimezidi kwa kuamua mwenyewe kuingia katikati ya uwanja na kumsaka mwanawe kwa hasira akiwa na imani kuwa atamchukua kwa lazima. Hii ni ishara kuwa kuna mvutano kati ya wahusika hao ndio maana vita vimezuka kutokana na tofauti hizi, lakini Sufiyani anashindwa na kumpoteza mwanawe.

Akaua marijali
jumla elfu mbili
kufari wasihimili
mara wakakimbia (ubeti 467)

Majeraha ya Abdirrahmani yanaonyesha jinsi vita vilikuwa vikali hata kumlaza chini. Nabii alimtuma Sheikh Ali Haidar na kumpa watu wanne wanaojulikana kuwa na ubabe vitani. Ali Haidar aliwaongoza hawa wanaume wanne katika safari ya kumuauni Abdirrahmani, makundi mengine makubwa yakiwafuata nyuma baadaye. Makundi haya yalikuwa na kiongozi ambaye alikuwa amepewa wanajeshi mia tano kila mtu pamoja na farasi wakiwa wamebeba silaha za kutosha. Wengine waligawanywa kuwa upande wa kushoto, kulia, mbele na kati haya yote yakidhihirisha matayarisho yao vitani. Vilevile mkusanyiko wa wanaume wenye nguvu unadhihirisha vita kwani tumeelezewa katika utenzi kuwa, nabii alimwita kiongozi bwana Bashari na kumpa askari mia tano wenye ujuzi katika vita. Wote walijipamba kwa mapambo yao ya vita kisha wakaanza safari kwenda alikokuwa Abdirrahmani kumuauni (ub. 523- 529).

Vita vya awamu ya tisa vilianza baina ya wanajeshi waliotumwa na nabii dhidi ya wanajeshi wa Sufiyani. Mikidadi ndiye wa kwanza kupigana na kuwaua kwa kuwakata vichwa na kisha kumwendea bintiye Sufiyani na kumwambia kuwa arudi kwa mumewe kwani usaidizi mkubwa kutoka kwa nabii umefika.

Kangia akiwakata
akawapukusa vitwa
kama wembe ulopata
na nywele za kulegea (ubeti 623)

Sufiyani ajitayarisha kwa vita zaidi kwa kuagizia wanajeshi hodari kutoka makabila mbalimbali kwa mfano kabila la Azzan walioongozwa na Kahlan pamoja na wanajeshi wake elfu mia moja waliojiandaa kwa silaha na wengine wengi waliokuja na wanajeshi wao kutoka kwa kabila la Shemlani ambalo linajulikana kwa ubabe wao vitani. Sufiyani anapata matumaini ya kushinda hivi vita idadi ya wanajeshi ilipotimia elfu mia sita kwa jumla na kwa hivyo kuwa tayari kwa vita lakini hawakufaulu kupata ushindi. Kuhusika kwa Shemlani ami yake Sufiyani vitani kunaonyesha kuwa vita hivi vilihusisha pia jamaa zake hivyo basi kudhihirisha wazi kuwa uadui huu ulikita mizizi miongoni mwa wanajamii.Vilevile kubadilishana kwa majeshi hawa vitani kunaonyesha jinsi vita hivyo vilikuwa vikali.

Idadi yao sufufu
sita miaati alfu
na mukadamu dhaifu
jina lake tawambia (ubeti 740)

Vita katika awamu ya kumi vilianza pindi tu Abbas alipowasili kukabiliana na kafiri Shemlani. Uwepo wa shujaa huyo kutoka kwa nabii ulichochewa na majigambo yake Shemlani yaliyodai kuwa shujaa huyu hawezi chochote hata akiingia uwanjani hivyo basi akaitwa ili kuonyesha ubabe wake vitani. Nguvu zao zilikuwa karibu kwenda sambamba hatimaye wanajeshi wa Sufiyani elfu arubaini wakauawa na upande wa nabii mia tatu ishirini. Vita huleta hasara isiyokadiriwa bila kubagua wahusika ndio maana wahusika wa vita hivi kutoka pande zote waliathirika. Makafiri waliouawa walienda motoni kutokana na imani yao hafifu isiyoamini Mungu. Waislamu waliouawa walirithi ufalme wa peponi kwani walishiriki vita takatifu.

Wafu wao islamu
thalatha mia timamu
na ishirini kutimu
wakenda fanya alama (ubeti 837)

Awamu ya kumi na moja ya vita ilitimia majeshi kutoka pande zote yakasitisha vita na kupelekea mauaji zaidi kupiku vita vya awamu zote. Vita hivi vilikuwa vikali mno ndio maana wanajeshi wengine hodari kutoka upande wa nabii wakaongezwa, Kaaba na Kinana waliosilimu wakiwemo. Damu ilimwagika hata kuwafika magotini.

Harubu ikakawia
damu ikenda milia
viumbe wakangamia
kupita harubu pia (ubeti 844)

Dua walioombewa kutoka kwa nabii ilionyesha jinsi vita katika hii awamu ya kumi na moja vilikuwa vinawawia vigumu hivyo basi nabii akawaweka mikononi mwa Mola na hatimaye wakawaua wapinzani wao kama maua yaliyopigwa na radi.

Tembe moja hujigawa
watu kumi ikaua
wakafa kama maua
ya wingu lakulemea (ubeti 926)

Mauaji dhidi ya upande wa Sufiyani yaliongezeka, wanajeshi karibu wote wa Sufiyani wakiuawa na kisha Sufiyani pamoja na Shemlani wakashikwa na kupelekwa kwa nabii kwenda kukiri imani ya Uislamu sawia na wanajeshi wake walionusurika kifo lakini walikataa katakata na mwisho kukubali kuuawa. Vita hivi vya kidini vilifikia kilele chake, upande wa Abdirrahmani wakichukua ushindi na kuishi Madina kwa amani pamoja na waliosilimu. Kilele cha vita hivi kinaonyesha matokeo ya mwisho kwa wahusika na ambayo yalikuwa ni vifo, kusilimishwa kwa makafiri hawa na kupelekwa Madina ( ub.964 -969).

Wahusika katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* wanaonyesha jinsi vita vya maneno huchangia vita vya silaha. Majigambo na vitisho vinadhihirisha ujasiri wa wahusika katika harakati za kupimana nguvu kwa mfano mwanajeshi hodari wa Sufiyani aitwaye Kinana anathibitisha hali ya kukithiri kwa vita pindi tu anapojitokeza uwanjani na kujigamba kuwa anamtaka shujaa wa nabii - Mikidadi anayejifanya shujaa ilhali hawezi lolote kuja na ndio ikawa mwanzo wa majibizano makali baina yao yaliyopelekea vita hatimaye. Haya mapigano ya maneno yaliendelea kutokea miongoni mwao kabla ya kila awamu ya vita vya silaha kuzuka. Mikidadi naye anajigamba kwa kusema kuwa, atamwonyesha vita vikali ambavyo hataviamini kwa hivyo anamuonya ajihadhari naye (ub. 643- 645).

Takuonyesha harubu
iliyo kubwa ajabu
ama upesi nijibu
Mikidadi kamwambia (ubeti 645)

Vitisho katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* vinaonyesha kuwa kuna uhasama unaotokana na tofauti za kidini na ambazo zimesababisha vita. Mhusika Kinana anatishiwa na nduguye Kaaba asishiriki vita dhidi ya shujaa wa vita aliyetumwa na nabii kwani anamfahamu kwamba hakuna anayempiku hivyo basi kupatwa na woga wa kuangamizwa na Mikidadi ndiposa wakaamua kusilimu ili kukwepa ukatili ambao wangetendewa vitani.

Maana hutamweza
usitake jangamiza
ukenda ukajisoza
tambua hutarejea (ubeti 658)

Shemlani anathibitisha kuwa kuna vita baina ya pande mbili anaponena kwa majigambo kuwa anamtaka mwanajeshi wa nabii Abu Fadhili aende alipokuwa ili amuonyeshe ukatili alionao jambo ambalo liliendeleza vita vya maneno baina yao na mwisho kuzua vita vya silaha vya awamu ya kumi ( ub. 771-772).

Wanajeshi wa Sufiyani na wa nabii wanakusanywa na kupewa maagizo kabla ya kwenda vitani. Hili linaonyesha jinsi wanavyojiandaa vitani licha ya kuwa na silaha zao lazima kuwe na kiongozi atakayeongoza msafara wa majeshi haya ili kuzuia uvamizi wa ghafla kama mbinu ya kukabiliana na adui.

> Hata usiku yuwani
> jamii masultani
> wakakutana khemani
> maamiri wote pia    (ubeti 746)

Kutubu kwa wanajeshi wa Sufiyani baada ya kushindwa vita kunaonyesha kilele cha vita vya kidini na vilevile kushikwa kwa kiongozi wao Sufiyani na mwanajeshi wake hodari Shemlani ni ishara ya kuisha kwa vita kwa hivyo ushindi wa Abdirrahmani dhidi ya Sufiyani ukadhihirika kupitia vita vya maneno na silaha. Kwa kawaida katika fasihi, Mhusika nguli anapoondolewa hadithini, matukio ya kazi ya fasihi yanakosa mtiririko unaofaa. Abdirrahmani na Sufiyani ndio wahusika nguli katika utenzi huu. Wahusika hawa wanafikisha kisa hiki mwisho wake baada ya Sufiyani kuuawa vitani hivyo basi hadithi hii inafika mwisho (ub.948 -950).

### 3.1.7 Maridhiano

Maridhiano ni kurudiana kwa mtu au jamii na kuwa pamoja tena baada ya kutengana kutokana na tofauti fulani iliyoletwa na kitu au jambo fulani hususan ugomvi, chuki au vita. Maridhiano hupatikana baada ya masikilizano au maelewano kuafikiwa hivyo basi makubaliano hufanya wahusika husika kuungana pamoja.

Maridhiano yanajitokeza katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* hasa pale ambapo mhusika mkuu Abdirrahmani anapotea akiwa na umri mdogo na kwenda kuishi na Sufiyani aliyeabudu miungu lakini baada ya kukosana na kiongozi huyo aliamua kurudi kwa wazazi wake Madina na kuridhiana nao licha ya kuwa alikuwa mwovu kupita kiasi. Maridhiano hayo ndiyo yalikuwa furaha kwa wazaziwe

waliokuwa wakisononeka walipokuwa wakipata habari kuwa Abdirrahmani aliwadhulumu wapita njia na watu wote katika nchi nzima.

Neno alilolileta
najuta sasa najuta
baba yangu kamuata
haja huku hapotea (ubeti 222)

Kuna maridhiano ya dini kutoka kuabudu miungu hadi kuabudu Mungu. Abdirrahmani kurudiana na wazazi wake ilikuwa ishara tosha kuwa ataisaliti au ataiasi imani ya miungu pindi atakapoachana na Sufiyani jambo ambalo lilitimia baada ya Mora kumpa waraka kutoka kwa babaye ujumbe ukiwa ni kumsihi aachane na dini ya uongo na kumrudia Mungu. Maridhiano hayo yalileta amani katika nchi zote kwani Abdirrahmani ndiye alikuwa ameteuliwa na Sufiyani kumchumia mali kupitia njia ya kuwadhulumu watu hivyo basi uvamizi huo dhidi ya watu ungefikia mwisho wake.

Maana kusema hayo
hii dini ya babayo
nimeitoka sinayo
tena nimeikataa (ubeti 239)

Kwani si dini ya ndia
ndipo nikaikimbia
na tena imenijia
khati ya baba sikia (ubeti 240)

Shamti bin Khadafu anaridhiana na mwanawe baada ya kuzuiliwa na Abdirrahmani ili Shamti alete yale aliyomwagizia lakini baadaye anamhurumia na kumwachilia huru jambo ambalo lilikuwa limeingiliwa kati na nabii Muhammadi aliyemwombea dua Shamti kwa minajili ya mwanawe aliyekuwa amefungwa. Hatimaye Shamti akaridhiana na mwanawe kwa furaha.

Tumwa kuonana naye
yu pamoja na babaye
akafurahi rohoye
mtume wetu rasua (ubeti 183)

Kinana na nduguye Kaaba wanaridhiana na wanajeshi wa upande wa Abdirrahmani baada ya kuona wanawazidi kwa nguvu. Ndugu hawa wawili ambao ni wanajeshi hodari wa Sufiyani wanagundua kwamba kushindwa kwao vitani ni kutokana na nguvu za Mungu hivyo basi wakaamua kusilimu na kukiri imani ya Uislamu na kuungana nao pamoja licha ya kuwa na uhasama baina yao hapo awali.

Kwisha silimu Kinana
na nduguye akanena
naweleza lake jina
nanyi mpate mjue (ubeti 677)

Jina aitwa Kaabu
ali shujaa ajabu
kashahadia wahabu
kauli akaitoa (ubeti 678)

### 3.2 Hitimisho

Tumeweza kushughulikia kazi yetu kwa kina katika sura hii ya tatu kwa kuchambua maudhui makuu yanayojitokeza katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Uchambuzi huu umezingatia misingi ya nadharia ya uyakinifu wa kijamii na kupitia nadharia hii,tumeweza kuhakiki na kuthibitisha maudhui kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano. Maudhui haya yanajitokeza wazi katika maisha ya binadamu ya kila siku popote pale walipo kwa hivyo uyakinifu wa maudhui haya yanadhihirika. Kuna mwingiliano mkubwa wa maudhui haya yote katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwani visa vyote vinavyotendeka kwenye hadithi vimesababishwa na dini hivyo basi dini imekuwa kama kiini au chanzo cha masuala mengine kutendeka. Suala la dini ndilo limezua usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano pamoja na maudhui mengine madogo madogo ambayo yamebebwa na maudhui makuu.

Maudhui haya yanaonekana wazi katika maisha ya jamii katika pilkapilka zao za kukidhi mahitaji yao ya kila siku kwani binadamu hutawaliwa na masuala matatu; masuala ya kijamii kama vile dini, masuala ya kiuchumi kama vile kazi ya kuchuma riziki na masuala ya kisiasa yanayohusiana na uongozi. Masuala haya yote ndiyo huzua mtagusano wa wanajamii ambao matokeo yake huweza kuwa chanya au hasi hivyo basi kuleta maudhui yenye kujenga maadili na pia maudhui yenye kubomoa miongoni mwa wahusika.

Vilevile katika sura hii ya tatu, tumeweza kutaja na kueleza maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* na pia kutolea mifano mwafaka inayothibitisha maudhui husika kwa kunukuu ubeti mmoja au mbili kutoka kwenye utenzi. Tumeeleza maudhui yetu kwa kina kwa kuhusisha waliochangia katika kufanyika kwa matendo fulani katika kisa, kwa hivyo maudhui na wahusika ni vitu viwili ambavyo haviwezi kutenganishwa katika kazi ya fasihi kwani jumla ya yanayozungumziwa kwenye kisa ,huwa yametendwa na mhusika fulani. Sura ya nne itaonyesha uyakinifu wa maudhui haya makuu kwa kutathmini uyakinifu wake katika jamii ya sasa.

# SURA YA NNE

## KUTATHMINI UYAKINIFU WA MAUDHUI MAKUU KATIKA UTENZI WA ABDIRRAHMANI NA SUFIYANI KATIKA JAMII YA SASA

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangalia namna maudhui yanavyoibua matokeo chanya na hasi katika jamii ya sasa kwa kurejelea *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Maudhui haya tunayoyaeleza yanasawiri uyakinifu na uamilifu wa maisha ya wanajamii. Tunatalii namna maudhui haya yanavyojitokeza katika maisha halisi ya binadamu duniani.

Maudhui haya makuu yanaibua matokeo chanya au hasi miongoni mwa wahusika na ambayo huathiri wanajamii kwa njia mbalimbali katika harakati zao za kusaka mahitaji yao ya kimsingi. Tunarejelea harakati hizi za kujitafutia riziki za maisha kwa kuoanisha na maelezo ya Lucaks (1963) kuhusu uyakinifu wa kijamii. Kulingana na Lucaks (1963), uyakinifu wa kijamii huonyesha jamii hasa katika awamu zake za mabadiliko na pia katika ukamilifu wake kwani ukamilifu huu huafikiwa na jamii wanapoweza kukidhi mahitaji yao muhimu ya maisha kama vile lishe, usalama, uzazi, faraja za kimwili, burudani, utangamano na maendeleo.

Tunaangazia maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano. Tunaeleza jinsi maudhui haya yanaleta matokeo mazuri na mabaya katika jamii ya sasa kwa kurejelea *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kama kurunzi ya kazi yetu katika sura hii.

### 4.1 Dini

Dini ni asasi ya jamii inayohusiana na masuala ya kiroho au imani ya binadamu katika maisha anayoishi ulimwenguni. Asasi hii ni muhimu katika kuongoza matendo ya binadamu katika hali ya maadili hivyo basi dini huchangia maadili katika hulka za wanajamii. Imani ya binadamu hutegemea kiumbe mwenye nguvu na ambaye huwa ni mwelekezi wa waumini wake kulingana na sheria za dini hiyo kwa mfano dini ya Kiislamu inaamini uwepo wa Mungu mmoja na mjumbe wake Muhammadi.

Vilevile dini inayoamini katika miungu huegemeza imani yake kwa kiumbe fulani au pia sanamu.Dini ina umuhimu wake katika kunyoosha tabia za wanajamii hivyo basi inachangia katika kuleta miujiza, uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii na pia mabadiliko hasa katika hulka za wanajamii. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umesawiri suala la dini kwa mapana na marefu kwa kuangazia dini ya Kiislamu pamoja na ukafiri.

Kuna umuhimu wa kuzingatia masuala ya dini kwani kuna manufaa yake hasa kwa waja wote wanaonuia kuishi ulimwenguni kwa amani. Kutokana na dini ya Kiislamu, waumini wake wanapaswa kumuamini 'Allah' yaani Mwenyezi Mungu na mtume wake wa mwisho Muhammadi. Kila jambo linalotendwa na waumini wake linafaa kuongozwa na imani ya Uislamu na ndio maana katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* mtunzi anaanza hadithi yake kwa kumshukuru Mungu na kumwomba amwongoze katika kazi yake ya uandishi au masimulizi.

Bismillahi nandike
'rRahmani Yu Pweke
Rahimu zote zi kwake
wajawe hutuletea (ubeti 1)

Kuanza kwa kumtukuza Mungu kunaonyesha umuhimu wa dini katika kumpa mja nguvu na matumaini ya kuendelea kufanya kazi yake kwani ndiye mwenye uwezo wa kuongoza matendo ya binadamu duniani. Jamii ya sasa pia imeegemeza imani yao kwenye kiumbe mwenye nguvu kuwapiku ndiposa kila dini duniani humwomba kiumbe huyo kabla na baada ya kufanya jambo kwa mfano dini ya Kiislamu hivyo basi dini hujenga matumaini katika maisha ya wanajamii katika kuendeleza shughuli zao za kila siku bila kukata tamaa.

Dini hutumiwa kama chombo cha kusuluhisha matatizo yanayokumba jamii. Jamii ya jadi na sasa hufanya dini kipengee muhimu cha kutatua changamoto zinazowakabili panapokuwa na tofauti zao zitokanazo na masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika shughuli zao za kusaka riziki au kukidhi mahitaji yao ya kimsingi.

Wahusika hawa wawili Kinana na Kaaba katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* walipoona vita vimekithiri na hawakuwa na njia nyingine ya kuweza kuwapiga wapinzani wao, waliamua kusilimu ili kuepuka kufa au kupata majeraha hivyo basi kukiri imani hiyo kama njia ya kusuluhisha tatizo lao.

Imani katika dini hasa ya Uislamu husaidia jamii katika kukuza maadili na kuhifadhi amali au tamaduni za jamii. Achieng (2012) anaeleza kuwa dini ni suala muhimu katika kukuza tamaduni za kidini ambazo jamii hukua nazo na kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Jamii ya sasa hukua kwa kurithi amali au tamaduni hizo walizozipokea kutoka kwa kizazi kilichopita hivyo basi hulka zao huandamana na maadili ya wanajamii wa jadi kama yanavyoelezwa kwenye kisa hiki.

Maadili yamejitokeza katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* miongoni mwa wahusika kama vile Abubakari na familia yake. Abubakari anadhihirisha maadili kwa kulea jamii yake kwa njia ya kidini Abdirrahmani akiwemo kabla ya kuasi dini ya Kiislamu jambo ambalo halikumfurahisha babake hata kumtafuta na kuridhiana naye katika dini ya kweli. Mora pia anathibitisha uadilifu wa Abubakari pindi tu walipokutana kwa mara ya kwanza njiani kwani maadili hujenga sura ya nje ya mtu yeyote yule.

> Yule mtu akasema
> Ya Shekhe neleze mwema
> naona u mtu mwema
> kwa umbolo na tabia (ubeti 107)

Dini pia hujenga uhusiano mwema katika jamii ya sasa. Kufaana katika jamii ndilo jambo muhimu kwa waja wote linalowaleta pamoja ili kusaidiana panapokuwa na mahitaji hivyo basi urafiki hudumishwa kupitia utangamano huu. Uhusiano mwema ulileta urafiki kati ya Abubakari na Mora hata Abubakari kupata msaada wa kumsaka na kumregesha mwanaye aliyekuwa amepotea akiwa na umri mdogo. Mora alitumia mbinu zake hadi akamshawishi Abdirrahmani kurudi kwao Madina.

Mwarabu anawasilimisha watu wengi katika jamii yake baada ya kukiri imani ya Uislamu hii ikichangiwa na ule uhusiano mwema na urafiki alionao katika jamii kwani watu wake hawengeitikia mwito huo pasi urafiki wa dhati.

Vilevile, katika jamii sasa, masuala ya kiroho yanahitaji uaminifu. Uaminifu wa mhubiri ndio hujenga uhusiano mzuri wa watu ili waweze kushawishika na kukubali dini hiyo kwa mfano dini ya Kiislamu ina mafundisho yake kabla ya mtu kusilimu. Maadili hujengeka katika jamii kupitia dini hivyo basi kuleta uhusiano mwema na amani miongoni mwa wanajamii wa sasa.

Umuhimu huu wa dini kufanya miujiza umerejelewa pia katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* pale ambapo Abdirrahmani anatumiwa uponyaji wa papo kwa hapo kutoka kwa nabii Muhammadi kupitia Sheikh Ali walipokuwa vitani (ubeti 622). Miujiza inatendeka vitani baada ya nabii kutuma nguvu za kumuauni Abdirrahmani. Nguvu hizi zilitoka kwa Mola kupitia kwa nabii ambapo anawatuma majeshi walio na ushujaa wa kupigana vitani ili kuendeleza vita dhidi ya Sufiyani. Baada ya makafiri hawa kushindwa vitani, waliweza kugundua na kuamini tofauti ziliopo baina ya dini ya kweli na uongo hivyo basi kujenga imani yao kupitia dini ya Kiislamu ambayo ina uwezo wa kufanya miujiza (ubeti 665 – 669).

Jamii ya sasa inatumia dini kuleta uaminifu hasa panapotendeka miujiza inayohusiana na masuala ya kiroho. Imani ya dini ya kweli hujengeka kupitia matendo ya kweli yanayoshuhudiwa katika sehemu yoyote ile patakatifu kwa mfano miujiza ya uponyaji baada ya maombi au sala.

Dini huleta mabadiliko ya mienendo ya wanajamii. Mabadiliko haya miongoni mwa wanajamii huafikiwa baada ya mhusika kuwa na imani juu ya kitu fulani au ushawishi wa jambo fulani linalomfanya kuamini analoona au linalotendeka. Imani ni masuala ya kiroho yanayohitaji thibitisho fulani ili mhusika aweze kujenga imani kwa mfano kusilimu kwa mtu au kuwa mkristo kunahitaji ushawishi wa hali ya juu. Mhusika Shamti bin Khadafu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* anaamua kuacha mali yake yote na kuamua kusilimu baada ya kung'amua kuwa bila dini hakuwa lolote ndiposa suala la imani likamjia na kubadilisha mienendo yake kuambatana na dini ya Kiislamu (ub. 47).

Kinana na Kaabu wanabadili imani yao ya kuamini miungu na kuamua kusilimu. Mienendo yao ya hapo awali yanabadilika na kuambatana na mafunzo ya Uislamu hivyo kuishi Madina kwa amani na kutangamana na waislamu wenzao.

Vilevile Abdirrahmani anabadilisha imani yake ya kuamini miungu baada ya babake Abubakari kumsihi na kumwombea kwa Mola aiasi dini hiyo na kurejea katika dini ya kweli na hatimaye akaridhiana na dini ya kweli aliyokulia akiwa mdogo. Mabadiliko haya ya hulka mbaya zamani ya kudhulumu nchi zote na hasa wapita njia zilitupiliwa mbali na kuwa mwema hivyo basi dini huleta mabadiliko ya kitabia.

Kuacha unyang'anyi kunaonyesha jinsi watu katika jamii ya sasa huweza kubadilisha mienendo yao ambayo huleta mikinzano miongoni mwao baada ya kuokoka kwa wakristo au kusilimu kwa waislamu. Mienendo hasi katika jamii huleta utengano na chuki na mwishowe kuzua vita kama ilivyokuwa katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* (ub. 977).

Jamii ya sasa hupata mabadiliko ambayo si haba kutokana na utandawazi au mtandao unaorahisisha mawasiliano na kwa hivyo usambazaji wa mila na desturi kutoka nchi zingine unaleta mabadiliko ya mienendo ya jamii ya leo ndio maana pasipo na dini inayoadilisha waja na kuleta mabadiliko yanayofaa katika malezi ya kizazi kijacho, maangamizi ya tamaduni yatatokea.

Imani ya Uislamu inapoleta mabadiliko na kuadilisha jamii, tamaduni za kidini zinahifadhiwa na kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kizazi cha leo kikihifadhi amali za jadi, kukuza kizazi kijacho kimaadili kutakuwa rahisi hivyo basi jamii ya sasa ina majukumu ya kulea vizazi vyote vijavyo kwani tamaduni hukuzwa kupitia kupokezanwa.

Abubakari katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* anawalea wanawe kwa njia ya uadilifu ingawaje, mwanawe anasaliti malezi yake bora na kuamua kuwa kafiri lakini kutokana na ule msukumo wa moyo wa kuhisi kuwa amemkosea babake, anatoka kwa Sufiyani na bila kurudi nyuma anaamua kupigana na bwana mkuu wake ambaye anamzuia kuondoka. Mabadiliko haya ya kitabia ya Abdirrahmani yanatokana na msingi wa utamaduni wa kidini ambao jamii yake ilikuwa imejenga ndio maana ushawishi wa Mora wa kumtaka arudi nyumbani kwa babake haukupokelewa vibaya hivyo basi amali ambayo babake alimlea nayo ilikuwa na msingi mzuri.

Dini huleta utulivu wa moyo baada ya jambo au tatizo fulani kutatuliwa. Binadamu huhitaji utulivu wa moyo ili aweze kupata nguvu ya kujifanyia kazi zake za kuchuma riziki ya kukidhi mahitaji yake. Jamii ya sasa imekumbwa na tofauti nyingi za kimaisha kutokana utangamano na mwingiliano wa kila aina za tabia kutoka kila jamii wanaoishi katika mazingira mamoja hivyo kuwa na mtagusano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii ambao kwa kawaida huleta mikinzano au mivutano inayosababisha vita na chuki. Utulivu wa moyoni miongoni mwa wanajamii ni silaha ya kuleta maendeleo. Shamti anakosa utulivu wa moyo jambo ambalo linamsababisha kuacha mali yake yote na kwenda kusaka ukweli wa dini ya Kiislamu baada ya kung'amua hana maana maishani bila uwepo wa dini kwani ndio huleta utulivu.

Haona ni kupotea
kuifuata dunia
ni dini isiyo ndia
ala isiyo shujaa (ubeti 45)

Jamii ya sasa hutumia dini kuleta amani katika nchi kwani madhehebu mbalimbali hubeba makabila yote nchini na ambayo yanashiriki pamoja makanisani au msikitini kama ndugu au jamaa moja hivyo basi kuondoa uhasama na kuleta umoja na amani katika jamii hasa katika mazingira yao wanamoishi.

Abdirrahmani anapoamua kuiasi dini ya kuabudu miungu anaandamana na makabila ya watu waliosilimu na kukiri imani ya Uislamu kutoka himaya hiyo na kwenda nao Madina na kuishi maisha yenye amani na utulivu tele. Dini ya Kiislamu hufunza waumini wake kuwa kila binadamu hupata malipo yake kulingana na maisha aliyoishi duniani kwa hivyo kuishi kwa amani duniani ni daraja la kuishi maisha mema baada ya kufa.

Kula mtu kagawia
pasiwe mlia ngowa
na mafungu sasa sawa
wote wakafurahiwa (ubeti 972)

Maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii huendelezwa kupitia dini. Jamii ya sasa huweza kupiga hatua kimaendeleo iwapo viongozi wanaoteuliwa kuongoza wananchi wana maadili. Suala la dini kama tulivyokuwa tumeeleza hapo awali ni kuwa jamii ya

sasa itapunguza ufisadi, udanganyifu, ubadhirifu miongoni mwa maovu mengine mengi yanayosawiriwa na viongozi wa sasa hivyo kuleta maendeleo katika uchumi wa nchi kwani ndilo suala muhimu linalotegemewa.

Jamii hujifunza kutokana na masuala ya jadi yaliyoleta maendeleo ili kujenga jamii ya leo kwa mfano baada ya Abdirrahmani kutoka kwa Sufiyani anayeabudu miungu, anajiepusha na unyang'anyi na dhuluma dhidi ya wafanyibiashara na wapita njia pamoja na nchi zote zilizokuwa zikidhulumiwa naye hivyo kupelekea kuwa na maendeleo katika nchi hizo. Mabadiliko hayo yalichangiwa na dini ya Kiislamu (ubeti 976 – 978).

Vilevile jamii ya sasa huweza kujifunza mengi kutokana na madhara ya matendo ya jadi yaliyofanywa na jamii hiyo na kuletea jamii nzima matatizo kwa mfano Sufiyani aliyeabudu miungu na kutendea watu maovu hatimaye akauawa sababu kuu ikiwa ukafiri wake. Jamii ya sasa inajifunza kutoka kwake umuhimu wa kuabudu Mungu badala ya miungu kwani baada ya kufa, binadamu hupata thawabu yake kulingana na matendo aliyoyatenda duniani kama vile Mikidadi alivyowahubiria Kinana na nduguye Kaaba ambao ni makafiri hadi wakakiri imani ya Uislamu. Suala la dini lina mafunzo kwa jamii ya sasa kwani watu wanapotenda dhambi duniani, wataenda jehanamu na wanapotenda mema wataenda peponi kuishi kwa raha hivyo basi kila binadamu ana wajibu wa kuchagua maisha atakayo duniani na akhera.

Mmekwisha nusurika
hata mbele ya rabuka
nyumba inayo majoka
hamu wenye kuingia ( ubeti 674)

Mtakwenda panda dari
za lulu na majohari
muwaoe na mahuri
kwa amriye Jalia ( ubeti 675)

### 4.1.1 Usaliti na Dhuluma

Katika sura ya tatu tumeeleza kwa kina jinsi usaliti huchangia pakubwa katika kuleta dhuluma katika jamii. Kwa kurejelea jamii ya jadi kupitia historia ya Abdirrahmani na Sufiyani, tunapata kujua kuwa usaliti na dhuluma ni masuala ambayo hayawezi

kutenganishwa katika hulka za binadamu wanaosawiri sifa hizi lakini huweza kubadilishwa na dini kama vile Abdirrahmani.

Usaliti na dhuluma zimeweza kuleta mtazamo tofauti kwa kutumia dini kubadili tabia hii hasa katika jamii ya sasa ambayo inakumbwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Jamii ya sasa ina jukumu la kuchunguza tabia zinazopatikana miongoni mwao ili kuwabadilisha wanaokiuka amali za jamii ambazo zimerithiwa kutoka kwa jamii ya jadi. Wahusika ambao wana tabia mbaya katika familia hugharimu mzazi fedha na wakati mgumu katika kusuluhisha madhara wanayosababisha dhidi ya wanajamii wenzao hivyo basi kumfanya mzazi kuweza kujukumika katika kunyoosha na kufunza wanawe maadili.

*Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umeonyesha jinsi usaliti na dhuluma hugharimu wazazi wa wanaodhulumu wenzao katika jamii kama vile ilivyomgharimu Abubakari kufunga safari ya kwenda nchi nyingine kumsaka mwanaye aliyekuwa akidhulumu watu mali zao na mpango wa kusafiri ulitokana na nabii kumtumia ujumbe wa kumsihi afanye hivyo ili kujukumikia madhara aliyoyafanya Abdirrahmani dhidi ya wafanya biashara na wapita njia ( ubeti 18 -19).

Kutokana na usaliti na dhuluma inayosawiriwa katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*, jamii ya sasa inaweza kung'amua kuwa matokeo yake ni hasi na huleta chuki, mauaji na vita katika jamii hivyo basi kuepuka tabia kama hii kabla ya hatari (ubeti 361- 405).

Jamii ya sasa hupata kujua kuwa usaliti na dhuluma hurudisha maendeleo ya nchi nyuma kwani jamii inapokosa amani, kazi au shughuli zao za maisha haziendi sambamba mfano mwafaka ukirejelewa pale ambapo wanabiashara wanatekwa nyara na kunyang'anywa mali zao na Abdirrahmani hivyo kuleta majuto katika jamii nzima. Vilevile, jamii ya sasa hujifunza kuwa vita vinavyotokana na usaliti na dhuluma huleta vifo bila kubagua kabila, dini na pia umri hivyo basi wanapaswa kujiepusha na mambo yanayoweza kuwaingiza katika vita.

### 4.1.2 Ndoa na Mapenzi

Ndoa ni asasi muhimu katika maisha ya binadamu ambayo huendeleza jamii kukua katika msingi wa familia. Muungano huu wa mume na mke katika kuendeleza na kupanua jamii yao ni zawadi kutoka kwa Mola hivyo basi inapaswa kujengwa kwa msingi wa kidini. Shabaan (1966) katika *'Pambo la Lugha'* anaeleza kuhusu manufaa ya kuwa na maadili katika maisha ya binadamu. Kulingana na Shabaan (1966) katika *Utenzi wa Adili*, kumcha Mungu ni jambo la muhimu hasa katika kuelekeza mtu kuwa na heshima kwa wazazi na pia kuwa na mapenzi ya dhati katika ndoa. Anamweleza mwanawe Adili azingatie sana suala la dini kwani ndilo chanzo cha kuwa na maadili katika ndoa.

Kulingana na maelezo haya, mawazo yetu pia yanaafikiana kwani tunavyojua katika maisha ya sasa ni kuwa, ndoa hudumu kwa amani panapotawaliwa na mapenzi ya dhati baina ya mume na mke. Dini huadilisha ndoa katika jamii ya sasa kama vile ilivyosawiriwa katika baadhi ya wahusika katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwa mfano Abubakari na mkewe, Abdirrahmani na mkewe binti Sufiyani na wahusika wengine waliosilimu ambao hawakutajwa kwa majina.

Asasi ya ndoa huipa jamii ya sasa mafunzo kwa kila jambo linalomhusu binadamu kwa hivyo kuendeleza na kuimarisha imani yao zaidi kwa Mungu. Abubakari na mkewe wanaonyesha jinsi ndoa yao imejengwa kwa msingi wa dini anapomwambia mkewe amwombee kwa Mola kwa minajili ya safari aliyokuwa nayo ya kwenda kumtafuta mwanawe Abdirrahmani (ubeti 93 - 97).
Ndoa huonyesha jamii ya sasa kuwa mtu hawezi kuishi pekee bali huhitaji msaidizi ili aweze kukidhi mahitaji ya hisia zake za kimwili, kuondoa upweke na pia kuendeleza kizazi cha jamii.

Wanajamii wa leo wanafaa kuelewa umuhimu wa kuwa na ndoa halali ili kujiepusha na magonjwa ya kisasa yanayoendelea kuchipuka kutokana na kukithiri kwa uasherati. *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umeonyesha ndoa yenye mapenzi ya dhati kama vile ndoa baina ya Abdirrahmani na binti Sufiyani kwani waliweza kushirikiana na kutiana moyo hasa walipokumbwa na uvamizi uliosababisha vita. Mkewe Abubakari anamwombea mumewe anapokwenda safari ya mbali.

Changamoto zinazokumba ndoa hasa za jamii ya jadi zinasaidia ndoa katika jamii ya sasa kufahamu na kuwa tayari kukabiliana nazo kwa kutumia hekima ili kuafikia suluhu bali sio kutalikiana kama ilivyozidi katika jamii ya sasa. Jamii inapasa kufahamu kwamba maadili yatokanayo na dini ndio hudumisha ndoa kuwa imara.

Tatizo lingine katika ndoa ya jadi lilisababishwa na wazazi hasa walipokuwa wakiwakataza binti zao kuolewa na waume waliowachagua wenyewe pengine kutokana na historia mbaya ya ukoo wao n.k. Mhusika Sufiyani katika *Utenzi wa Abdirrahamani na Sufiyani* anamkataza bintiye kwenda na mumewe Madina bila kujali kuwa mapenzi ni uteuzi wa moyoni ( ub, 251).

Jamii ya sasa bado inakumbwa na changamoto sawia na za jadi zinazosababishwa na wazazi. Wazazi wengine hukataza binti zao kuolewa na waume wasiomudu kulipa mahari. Wazazi wa sasa hutaka mahari ya kiwango cha juu hivyo kufanya wachumba wa binti zao kushindwa kulipa na hatimaye kuachana nao. Vilevile jamii inajifunza kuhusu umuhimu wa kujenga ndoa yao katika msingi wa mapenzi ya kweli ili panapotokea jambo linalotishia kuleta utengano, waweze kusimama imara.

### 4.1.3 Ushujaa

Maelezo yetu katika sura ya tatu yalibainisha wazi kuwa shujaa ni mtu jasiri asiye na woga wa kutenda jambo. Majagina wa jadi walijulikana kwa sifa za ushujaa ambazo sifa hizo hazikupatikana katika binadamu wa kawaida. Majagina hawa walipitia changamoto mbalimbali za maisha hasa katika harakati zao za kupata ukombozi kutokana na hali dhalilishi, haya ni kwa mujibu wa Mberia (1989).

Ushujaa una umuhimu wake hasa katika kuleta uhuru au ukombozi kutokana na hali dhalilishi zinazorudisha maendeleo nyuma kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mashujaa hawa wanaweza kuonyesha ubabe katika hali mbalimbali za maisha hivyo basi kubainisha mashujaa wa kidini, kivita na kadhalika.

Mashujaa katika jamii wana umuhimu kwani wanasaidia katika kukidhi mahitaji ya jamii yanayohitaji utatuzi wa aina fulani. Mashujaa walikuwepo katika kila jamii ya jadi na walijulikana kwa sifa zao bainifu ambazo zilikuwa zikifanana. Hadithi za

mashujaa zimekuwa katika historia na kupitishwa kwa jamii ya sasa kama njia moja ya kuunganisha jamii ya jadi na sasa.

*Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* umesawiri mashujaa mbalimbali wa kidini na vita walioonyesha ubabe wao katika shughuli zihusianazo na uchumi, siasa na jamii. Mashujaa hawa wana umuhimu wao kwa maisha ya jamii ya sasa ingawaje waliishi katika jamii ya jadi kwani mambo mengi yanayotendeka sasa yanarejelea matukio ya jadi isipokuwa katika mambo machache ambayo yanapata mabadiliko kutokana na kukua kwa jamii ya sasa kiteknolojia.

Ushujaa wa jadi unaoelezewa katika jamii ya sasa husaidia katika kujenga imani ya dini hasa mashujaa wa kidini walioishi na kutenda miujiza kadha wa kadha katika dini ya Kiislamu pia ya Kikristo. Wanajamii wa sasa wanaegemeza imani yao kwa Mungu kupitia shujaa wa dini aliyepewa uwezo mkubwa wa kufanya miujiza kwa binadamu ili waweze kuamini uwepo wa Mungu. Bibilia imeonyesha Yesu kama shujaa wa kidini sawia na Qur'an inavyoeleza kuhusu nabii Muhammadi na miujiza aliyoifanya.

Nabii Muhammadi anamwombea mwanawe Shamti aliyekuwa ametekwa nyara na Abdirrahmani na mwishowe kuachiliwa bila kudhurika. Vilevile, uponyaji wa papo kwa hapo dhidi ya Abdirrahmani unaonyesha ushujaa wake wa kidini ambao waumini wa sasa wa dini ya kiislamu wanajenga imani yao kupitia yeye hivyo basi nabii Muhammadi anabaki kuwa daraja la kumfikia Mungu kwani ndiye mwombezi. Jamii ya sasa bado inaamini kuwa Muhammadi ndiye atakayewaombea Waislamu kwa Mungu siku ya mwisho.

> Wewe ndiwe muombezi
> kesho mbele ya Aziza
> na tena ndiwe mpenzi
> kipendo chake Jaliya (ubeti 39)

Kupitia ushujaa huu wa nabii Muhammadi, jamii ya sasa imepata kuhifadhi historia yake na ambayo itapokezwa kwa jamii ijayo. Historia hii inadumisha tamaduni za kidini ili kizazi kijacho kipate ukweli wa dini ya Kiislamu kutokana na historia hii inayorejelewa kila siku katika mafunzo ya dini msikitini.

Jamii ya jadi na sasa hutumia ushujaa kutosheleza masuala yaliyohitaji na yanayohitaji sasa suluhu mwafaka. Mashujaa wa kale ndio waliweza kujenga mashujaa wa sasa katika jamii kwa sababu watu wanatatua matatizo yao yanayowadhalilisha wakiongozwa na kiongozi ambaye ni jasiri na hana woga wa kufanya mambo yanayokomboa jamii yake kwa mfano jamii ya sasa inakumbwa na ufisadi na kwa hivyo mashujaa wa sasa hukomboa hali kama hii kupitia kufichua ufisadi na hata pia kuongoza maandamano kama njia ya kutafuta kusikizwa na wanaowatawala.

Abdirrahmani katika *Utenzi wa Abdirahmani na Sufiyani* anaonyesha ushujaa wa kivita kwa kupigania haki yake dhidi ya hali dhalilishi inayomzuia kuridhiana na babake mzazi pamoja na dini yake ya awali hivyo basi kutetea haki yake ili kuleta ukombozi kwa jamii nzima. Uhuru aliokuwa akiusaka umesaidia makafiri kukiri imani ya Uislamu na kuishi maisha ya raha.

Majina ambayo jamii ya sasa huwapa watoto wachanga hutokana na mashujaa walioishi katika jamii. Majina haya yanaaminika kujenga hulka au maadili ya jamii kuambatana au kufungamanishwa na mhusika aliyekuwa na sifa nzuri kwa mfano jina Abdurrahmani hutumiwa katika dini ya Kiislamu hivyo basi historia ya ushujaa hutambulika kupitia jina hilo na ndio maana wazazi wa leo hutafuta majina kwenye bibilia au Qur'an wakiamini majina yenye sifa nzuri hujenga maadili.

Maendeleo ya jamii ya leo hutokana na ushujaa kwa sababu tunapoangazia uchumi wa nchi unavyodidimia, mashujaa ndio huwa katika mstari wa mbele katika kuleta ukombozi kama vile Abdirrahmani alivyofanya katika kuauni jamii ya Sufiyani kupitia vita (ubeti 358 - 364). Mashujaa wa sasa wanaweza kupigania uhuru wa wananchi kwa kuiga matendo ya mashujaa wa jadi ili kuikomboa jamii dhidi ya hali dhalilishi kama vile ukabila, ufisadi na kadhalika. Vilevile mashujaa wengine wa vita kama vile Mikidadi wanasababisha maafa na machafuko mengi katika harakati za kuusaka ukombozi hivyo basi jamii ya sasa hupata funzo kuhusu madhara ya vita na kuepuka kwa kutumia mbinu ya mazungumzo katika kusuluhisha matatizo yao.

### 4.1.4 Vita

Vita ni hali ya kutumia nguvu kupigana kwa silaha au maneno baina ya sehemu mbili zilizotofautiana na kujenga chuki kati yao. Vita vilidhihirika katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kuanzia mwanzo hadi mwisho na kuleta matokeo hasi yanayoipa jamii ya sasa maadili fulani. Kwa kurejelea vita hivi, jamii hujifunza kuwa vita husababisha jamii kutengana na kuendeleza chuki miongoni mwao. Mfano katika hadithi ni pale Shamti bin Khadafu anakumbana na vita vya maneno dhidi ya Abdirrahmani anayemteka nyara na kumtishia kifo.

Vita hurudisha jamii nyuma kimaendeleo kwani jamii huchukuwa muda wao mwingi wa kufanya kazi kupigana na kusababisha maafa ya wanajamii ambao wangeimarisha uchumi kama ilivyokuwa katika kisa hiki ambapo Abdirrahmani na Sufiyani walipigana kwa zaidi ya siku kumi mfululizo.

Vita vikashikamana
Pasi nafasi kupana
hata kifika mchana
shujai kamtokea (ubeti 421)

Wakalala ni laili
kukisha siku ya pili
wakamkia kitali
jeshini mwao kangia (ubeti 425)

Vilevile vita husaidia jamii ya sasa kung'amua ukweli wa jambo fulani baada ya madhara yake kufanyika kama vile walivyofanya Kinana na Kaaba kusilimu walipogundua kuwa nguvu zitokazo kwa Mungu ndizo zimewashinda vitani.

### 4.1.5 Maridhiano

Maridhiano ni hali ya kurudiana na kitu au mtu baada ya kutengana naye kwa muda fulani kwa mfano wahusika kama vile Abdirrahmani anaridhiana na jamii yake pamoja na dini ya Kiislamu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Abdirrahmani pia anaridhiana na babake mzazi baada ya kumtoroka kwa muda mrefu na pia kutoroka kwake kulimfanya kwenda kuabudu miungu lakini baadaye anarudia dini yake ya kweli.

Jamii hupata mafunzo kutokana na historia kuhusu jamii ya jadi hasa kwa kufahamu kuwa panapokuwa na tofauti fulani miongoni mwao, pana haja ya kuridhiana kama njia ya kuleta amani katika jamii. Jamii huishi kwa umoja na upendo maridhiano yanaposisitizwa kati yao hivyo basi kuendeleza maendeleo.

## 4.2 Hitimisho

Jamii ya jadi imetumiwa na jamii ya sasa kama kurunzi ya kuelekeza hulka zao kwa kurejelea masuala muhimu yanayohitaji suluhu. Jamii ya jadi iliendeleza maadili na ilikuwa muhali sana kupata wanajamii wakipotoka na kuenda kinyume na tamaduni za jamii na iwapo ukosefu wa maadili ungeshuhudiwa, jamii ilijukumika katika kurekebisha wahusika hao kinyume na jamii ya sasa ambayo ubinafsi umewaingia na kila binadamu anajitegemea pasi kujali mja mwenzake. Kizazi cha leo hukumbwa na changamoto nyingi zitokanazo na maendeleo ya kiteknolojia hivyo basi suala kama dini linafaa kutumiwa kama silaha ya kutoa suluhu mwafaka.

Jumla ya masuala yote yanayorejelewa katika sura hii yana uyakinifu katika maisha ya binadamu katika jamii ya jadi na ya sasa. Tumeoanisha masuala haya katika nyakati zote za binadamu kwani yanafanyika katika maisha ya wanajamii popote walipo. Katika sura itakayofuata, tumehitimisha utafiti wetu kwa kupendekeza mada zingine zinazoweza kufanyiwa utafiti zaidi siku za usoni.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii ya mwisho, tumehitimisha utafiti wetu pamoja na kuthibitisha haipothesia zetu na vilevile tumependekeza pia mada zingine kwa wasomi wengine watakaonuia kufanya utafiti siku zijazo.

### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Tumeigawa kazi yetu katika sura tano na kila sura imebeba matini tofauti tofauti kuhusu utafiti huu. Katika sura ya kwanza, tumeangazia utangulizi wa utafiti wetu, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya kinadharia, mihimili ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu fasihi kwa jumla, yaliyoandikwa kuhusu mada na mwisho kabisa, mbinu ambazo tumezitumia katika utafiti wetu. Sura ya pili ya kazi yetu ina maelezo kuhusu viambajengo vinavyojenga na kuendeleza maudhui kama vile wahusika, mandhari, msuko, usimulizi na fani. Katika sura ya tatu, tumechambua maudhui makuu yanayojitokeza katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani*. Sura ya nne inahusu uyakinifu wa maudhui haya makuu katika jamii ya sasa.

Katika tasnifu yetu, tumechambua maudhui makuu katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Nadharia ya uyakinifu wa kijamii imetuongoza katika kuchambua masuala haya yanayogusia hali halisi ya maisha ya binadamu. Nadharia hii inalenga kuonyesha hatua ambazo jamii imepiga kimaendeleo hasa kisosholojia. Tumeeleza pia uyakinifu wa maudhui haya makuu katika jamii ya sasa kwa kuonyesha uhusiano uliopo baina jamii ya jadi na jamii ya sasa.

### 5.2 Matokeo

Tumeweza kueleza kwa kina maudhui ya dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa,vita na maridhiano katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Mtunzi ametunga utenzi huu kwa kuonyesha wazi maudhui au masuala yanayohusiana na binadamu katika shughuli zake za kila siku. Tumepata kuelewa zaidi kuwa maudhui yanajengwa na kuendelezwa na viambajengo kama vile mtindo. Mtindo hugusia

vipengele katika fasihi kwa mfano wahusika, mandhari, msuko, usimulizi na fani. Wahusika na sifa zao hujenga maudhui husika kwa mfano mhusika aliye na sifa ya kufanya mambo bila woga, hujenga na kuendeleza maudhui ya ushujaa.

Mandhari ambayo vitushi vinatendeka pamoja na wakati husika yametusaidia kubaini kipindi ambacho utenzi ulitungwa na mazingira maalum ambayo matukio yalifanyika. Msuko na usimulizi ni vipengele ambavyo mtunzi ametumia ili kuonyesha mtiririko wa yale msimulizi anaeleza na pia kutambua msimulizi kupitia nafsineni katika kisa hiki. Tumepata kujua kuwa, masuala haya yanayoonyeshwa na mtunzi yana uyakinifu katika maisha ya sasa ya wanajamii. Jamii ya sasa hukumbana na mambo yaliyotendeka hapo jadi kwa mfano usaliti na dhuluma, vita n.k. na kwa hivyo jamii hupata mwelekeo mzuri wa kuchunguza matokeo hasi yaliyotokea wakati huo ili kusuluhisha masuala yanayowakumba sasa kwa njia ya amani.

Tumeweza kuthibitishanadharia tete yetu ya kwanza kwa kuonyesha kuwa maudhui kuu ambayo ni dini, yamezaa maudhui mengine kama vile usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano. Pili, tumethibitisha nadharia tete ya pili ya kuwa maudhui yanayojitokeza katika utenzi wetu kama vile dini, usaliti na dhuluma, ndoa na mapenzi, ushujaa, vita na maridhiano ni masuala yenye uyakinifu katika maisha ya wanajamii kwani yanatendeka katika maisha yao halisi.

### 5.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Tunapendekeza watafiti wengine watakaojitokeza baadaye, waangazie fani katika *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* kwa kutumia nadharia tofauti tofauti katika kuchanganua kazi hii. Vilevile, wanaweza kuchunguza suala la dini ya Kiislamu kwa kulinganisha na dini ya Kikristo katika tanzu zozote zile katika fasihi kama vile riwaya, tamthiliya na tanzu nyingineo.

# MAREJELEO

Abdalla, H. (1891). *Utenzi wa Vita vya Wadachi.* Dar es salaam: Education Service Centre Ltd.

Abdalla,S. na Abdalla, H. (1961). *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Nairobi: K.L.B.

Abdilatif, A. (1973). *Fumo Liyongo.* Dar es salaam: Chuo Kikuu cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.

Abou, Egl, Mohammed. (1983) 'Life and works of Mohammed Kijumwa'. S.O.A.S, London. Unpublished PHD, Thesis.

Achieng,O. (2012). 'Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao kwa Jamii zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere'. Nairobi: (Haijachapishwa).

Biebuyck, P. na Mateene, C. (1969). *The Mwindo Epic.* California: Califonia University Press.

Brecht, B. na Bathrick, D. (1973). *Intellectuals and Class Struggle.* Germany: New Germany Critique.

Clark-Bekeleremo, J. (1991). *The Ozigi Saga.* Washington D.C.: Howard University.

Gatakaa, G. (2012). 'Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa'.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

Gorky,M. (1973). *The Lower Division.* The Viking Press.

Grass, G. (1962). *The Tin Drum. Tafsiri ya Ralph Manheim.* New York: Vintage.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry.* Oxford: The Claredon Press.

Kezilahabi, E. (1997). 'Creative Writing in Swahili. Makala ya Kongamano la Uandishi wa Ubunifu katika Lugha ya Kiafrika', SOAS, (p. 59). London.

Knappert, J. (1971). *Swahili Islamic poetry.* Leiden: E.J Brill.

__________ (1979). *Four Centuries of Swahili Verse.* London: Heinemman KL.

___________ (1967). *Traditional Swahili Poetry. An investigation into the concept of East Africa Islamic as reflected in the Utenzi Literature.* Leiden: E.J Brill.

Lucaks, G. (1963). *The meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili. Nadharia na Misingi ya Uchambuzi.* Dar es salaam: Mture Education Publishers Ltd.

Mayoka, J. (1978). *Utenzi wa Vita vya Uhuru wa Msumbiji.* Arusha: East African Publication.

Mbatiah, M. (2010). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine: Mambo muhimu katika uhakiki wa hadithi fupi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mdee, J.S. nw. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21,.* Longhorn Publishers.

Mghanga, J. (1984). 'Fasihi Simulizi katika Jamii, Uhakiki wa Ngano za Kidawida': Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

M'ngaruthi, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es salaam.

Ndumbu, J. (2013). 'Matumizi ya Takriri na Sitiari katika Utenzi wa Rasi' Lghuli': Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu Cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

Njogu. K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu.* Nairobi.

Owallah, K. (2013). 'Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Nabii Issa'. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

Robert, S. (1966). *Pambo la Lugha.* Nairobi: Oxford University Press.

________ (1968). *Utubora Mkulima.* London: Nelson.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi Andishi.* Dar es salaam: Kaultu.

__________ (1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es salaam: Press & Publicity Centre.

Swaleh, A. (1992). 'Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupona'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

Trimingham, J. (1962). *Islamic in East Africa,.* London: Edinburgh House Press.

Vutagwa, F. (2013). 'Sifa za Uhalisiajabu na Umuhimu wake katika Utenzi wa Mwana Fatuma'.Tasnifu ya Uzamili. Chuo cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

Wa Mberia, K. (1989). *Fumo Liyongo. Mulika* nambari ya 21., (pp. 25-43). Chuo Kikuu cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.

Wa Mutiso, K. (1985). 'Hurafa katika Utenzi wa Hamziyyah'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).

Wafula, R. & Njogu, K. (2007). '*Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi'.* Nairobi: Focus Publication.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi- Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide- Muwa Publishers Limited.

__________ (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

__________ (2003). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

__________ (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publication Limited.

Watuha, A. (2011). 'Maudhui ya Waadhi katika Utenzi wa Adili'.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: (Haijachapishwa).